

TANGU WAKATI HUO

 Ilikuwa ikifanyiwa kwenye mji mwingine hapa, kitu fulani kabla hatujaifanyia huko Grants Pass. Naye akaninii tu, mahali pengine huko Oregon. Nilikutana naye tu huko nje, nami... Unajua inakufurahisha kukutana na marafiki wa zamani tena, inanifurahisha mimi. Nami ninamwazia wakati wote. Alikuwa... kusimamia katika mikutano nikamwambia anapaswa kuwa humu ndani mapema kidogo, na tungemwomba aseme kitu.

Akasema, “Siwezi kuingia. Loo, ilibidi tu nishuke upesi kukuona.”

Nikasema, “Afadhali uingie.”

² Msisimko mwingine ambao umekuja tu dakika chache zilizopita, wakati Billy, mwanangu, aliponipa kifurushi kidogo. Nami na—nawaambia, ndicho kitu kitamu sana ambacho ni—nimekuwa nacho kwa muda mrefu kiasi. Kulikuwa na msichana mdogo hapa, nayo maskini nafsi yake ikachochewa sana, akanitumia sa—sadaka. Na endapo mawakala wa Shirikisho wanawazia nitawaonyesha hii, wamekosea. Nayo ina muhtasari kidogo hapa ulio mzuri kweli.

³ Anasema, kwamba, “Nakupenda sana. Nina umri wa miaka kumi na mitatu. Ninakupa sadaka hii. Niliipata kwa kuuza chupa. Mungu akubariki milele”: senti kumi na tatu.

⁴ Hilo lilikuwa zuri sana. Kamwe hakuandika jina lake, kasema, “msichana mdogo tu anayempenda Bwana.” Yeyote uliye, dada mpendwa, Mungu akubariki. Hiyo ni... Hujui hilo linamaanisha nini kwangu. Hiyo ni takatifu kwangu kadiri ya mtu kunipa noti ya dola mia moja mle ndani.

⁵ Nafikiri ilikuwa yule Gypsy Smith mashuhuri, katika kusoma baadhi ya muktadha wa hadithi ya maisha yake. Aliulizwa wakati mmoja ni msisimko upi mkubwa kuliko yote aliowahi kupata. Akasema, “Vema, walikuwa wakitaka kuchukua sadaka ya upendo kwa ajili yake usiku mmoja, naye alipokuwa akipanda vipandio vya nyuma akija,” akasema, “kulikuwako na maskini msichana mdogo mjipsi mchakavu amesimama pale.”

⁶ Naye akasema, “Bw. Smith?” Kasema, “Tumetoka kwenye familia maskini.” Kisha akasema, “Umemwongoza mama na baba yangu kwa Bwana Yesu.” Tena akasema, “Nilijua usiku wa leo ulikuwa wa sadaka yako ya upendo, nami sikuwa na kitu cha kukupa.” Akasema, “Ndipo mama mmoja leo akanipa pe—peremende kijiti nami sikutaka kuitia kwenye matoleo, Bw.

Smith, kwa hiyo ni—nikaifunga tu nikafikiria ningeкупа toleo langu mwenyewe.” Peremende kijiti ndogo, ya kumumunya.

⁷ Alisema alimazama maskini mtoto huyo mchakavu na kile kilichotukia. Unajua, hiyo inamaanisha, hiyo ni kutoka kwa moyo halisi. Unajua, hicho ni kitu kitamu na chenye mguso. Nami nadhani hapo ndipo maisha halisi yalipo, ni wakati yakiwa karibu na moyo.

⁸ Naweza kuwazia ki—kitu kidogo cha namna hiyo katika mmoja wa mikutano huko Finland. Samahani, ilikuwa huko... ndiyo, bado nadhani ilikuwa Finland; naam, ilikuwa, huko Kuopio. Sijaliwazia kwa muda. Kulikuwako na mvulana mdogo aliyefufuliwa kutoka kwa wafu, ambaye nilikuwa nimemwona katika ono miaka miwili (hapa Marekani) kabla ya kwenda nchi za ng'ambo.

⁹ Kunaweza kuwa na watu hapa ambao walinisikia nikilisimulia; nilikuja huku... Naam, kuna mikono mingi iliyoinuliwa. Kwamba nilisema, “Kutakuwa na mvulana mdogo mahali fulani, amelala ambapo pana miti, misonobari, na itakuwa miamba mikubwa imelundikana pamoja. Ndipo mvulana huyo mdogo atauawa katika ajali, naye Bwana Mungu atamfufua.”

¹⁰ Basi nilikuwa nikishuka kutoka kwenye mnara wa... Nitaninii... imekuwa muda mrefu; siwezi kulikumbuka jina la huo mnara. Ilikuwa huko juu kwenye... ilikuwa Kuopio, Finland, kama miaka kumi na miwili iliyopita, nasi tulikuwa tukishuka.

¹¹ Ford iliyotumika, ya karibu miaka sita au saba huko Finland, ingeuzwa kwa karibu dola elfu mbili na mia tano, labda elfu tatu. Na petroli ni senti tisini na tano kwa galoni. Kwa hivyo mahali kulipokuwa na angalau watu elfu ishirini na tano, thelathini na tano, ungeona yapata magari mawili au matatu. Na mle ndani, wa—wanapanda kitu kama sleji ndogo, kama mkokoteni, anaovaa Mhindi, anaendesha na, ama, alikuwa akiuendesha, kusafiri kwa mkokoteni, nao walikuwa na kuro aliyewavuruta kwenye mkokoteni huu. Halafu chini kwenye...

¹² Nilikuwa nimepanda gari juu ya kilima, na huko chini ulikuwa Kuopio, Finland, ninii... nilikuwa huko yapata majira ya Mei. Jua... Wana siku moja tu kwa mwaka huko, siku moja tu. Miezi sita jua limechomoza; miezi sita limetua. Na hii ilikuwa wakati tu jua lilipokuwa tu likitokeza kwenye upeo wa macho. Usiku wa manane, tungeweza tu... kuzuri na kwenye mwanga kama ilivyo hapa, kusoma gazeti usiku wa manane. Kisha linarudi tena. Nawe unaenda kulala tu unaposhikwa na usingizi; hivyo ndivyo unavyoidhibiti siku wakati jua limechomoza. Ndipo basi linatua kwa mwaka, au, kwa miezi sita. Halafu... Hiyo ni huko juu Lapland.

¹³ Basi tukishuka mlima ambako tulikuwa tukiimba, kulikuwa na—na Mwingereza mlevi kule juu. Hakujuu kilichokuwa kiki-...Alikuwa mnunuzi wa mbao kutoka Uingereza, naye alitaka kujua uimbaji huo ulihusu nini. Naye alikuwa katika hali mbaya kama nilivyo, mimi...Unapoweza kuzungumza Kifini, wewe ni mzuri sana, kwa sababu nadhani wana takriban herufi hamsini au sitini katika alfabeti, na kwa hiyo wao...Ni watu wazuri sana, baadhi ya watu wazuri sana niliowahi kukutana nao maishani mwangu. Nao walikuwa watu wa kupendeza sana.

¹⁴ Kwa hivyo basi, wakati nilipokuwa huko juu, Mwingereza huyu alikuwa anaendelea. Nami nikamwambia ulikuwa ni mkutano wa kidini. Nilimuuliza kama alimjua Bwana Yesu kama Mwokozi wake binafsi. Akasema hapana, hakujuu chochote kuhusu dini yoyote. Kwa hivyo hapo nilikuwa na majaliwa ya kumwona Bwana Yesu akimtoa ulevi mtu huyo na kumpa wokovu nafsiini mwake, tukapiga magoti kule nje kwenye matope na uchafu huko nje uani mwa mnara huu mkubwa, kwa namna fulani ni mnara wa ulinzi, mnara wa kale wa ulinzi. Na tulikuwa huko juu tukimsifu Mungu kutoka juu.

¹⁵ Nao wangeniambia jinsi Warusi wangeingia wakati wa vita na kurusha mabomu juu ya mji, kisha wanakuja juu ya mnara huo. Ndipo basi tungeweza kuangalia moja kwa moja kwenye hilo Pazia la Chuma hata Urusi, karibu maili mbili.

¹⁶ Tukishuka chini...Tulipokuwa tumekusanyika pamoja kuomba baada ya wao kumwona Mwingereza huyu...Nilikuwa nimeshuka chini huku nikitembea-tembea huko chini ya huo mnara, na—naye Ndugu Jack Moore alikuwa pamoja nami, naye Mwingereza huyu alikuwa ndio kwanza amjie Kristo. Wote wakashuka, ndipo kitu Fulani kikanijia kiajabu sana. Vema, walikipiga picha, ninayo nyumbani.

Nikasema, “Kumbukeni, jambo fulani liko karibu kutukia; ninalihisi tu. Kitu fulani kitatukia. Sijui ni nini.”

Kwa hivyo wakaanza kuuliza, “Kitakuwa nini?”

Nilisema, “Sijui. Ni jambo tu linalokaribia kutukia.”

¹⁷ Karibu maili moja chini ya kilima, tuliona mahali ambapo kulikuwa na Ford ya miaka mitano au sita iliyotengenezewa Marekani...Baadhi ya watu, waliokuwa juu ya kile kilima kwenye ule mnara walikuwa wameshuka, na watoto fulani wadogo wa shule walikuwa wakitoka shuleni. Nao...wazazi wao...Wanaishi mjini, kitu kama Ujerumani, wanaishi mjini, nao wanalima mashambani, kisha wanarudi mjini.

¹⁸ Wavulana wadogo wawili, mmoja mwenye umri wa karibu miaka tisa, na mmoja karibu, loo, ningesema, karibu umri wa miaka sita. Walikuwa wakivuka barabara, nalo gari hili likija kasi, wala hakuna magari, wao...ni vigumu kuyapata, hawakuwa wakitarajia gari. Nao maskini jamaa hao

wameshikana mikono, ndipo wakaona gari limetokea ghafla; ndipo mmoja akaenda upande mmoja, na mwingine kwingine. Nao walikuwa wameshikana mikono. Hatimaye, wakaachana mikono, naye mtu huyo, dereva, akachanganyikiwa, wala hakujua aende wapi, kwa sababu hao watoto walitorokea pande zote, akashindwa kulidhibiti gari.

¹⁹ Ndipo moja ya mabamba ya upande wa kushoto likamgonga mvulana mmoja katikati ya macho namna *hiyo*, na kumtupa juu, na kumgongesha kwenye mti na mshtuko wa ubongo na kuvunja mifupa yake. Ndipo huyo mwingine, lilimkanyaga moja kwa moja, namna *hiyo*. Likamkanyaga, kisha likamtupa, ambapo gurudumu la nyuma lilimpiga, likamvuruta kote barabarani hata nyasini. Hilo gari likakimbia kilimani, likajigonga kwenye lundo la mawe, likapinduka.

²⁰ Tulipofika kwenye eneo la tukio, kulikuwako na m—mtu mwingine, gari ambalo lilikuwa limefika hapo mbele yetu na kumchukua huyo mvulana mdogo aliyekuwa akipumua, likampeleka hospitalini mwao. Naye mkuu wa jiji, ambaye ni sawa na meya wa jiji, alikuwa huko, daktari alikuwa amekwenda huko, na . . .

²¹ Lakini sheria nchini Finland, kwamba wasingeweza kumwondoa mtoto huyu sasa, mpaka wazazi watakapokuja. Kwa hivyo walikuwa wameondoka wamepanda farasi, au, gari la farasi kwenda kondeni kuwatafuta wazazi wa huyo mtoto, wawalete.

²² Na vema, tukasimama. Ndugu Gordon Lindsay, shemeji wa Ndugu Hall, alikuwa hapo, Ndugu Ern Baxter, na Ndugu Jack Moore, na ndugu kadhaa; ndipo tukasimama. Naye Bibi Isaacson; anaweza akawa mumu humu kwenye mkutano huu usiku wa leo; anaishi hapa mahali fulani. Uko hapa, Dada Isaacson? Alikuwa mfasiri wangu wa Kifini.

²³ Na kwa hivyo, walishuka kutoka kwenye gari kumtazama yule mtoto mdogo kisha wakarudi. Tulikuwa tumeona ajali ilikuwa imetokea. Wakarudi wakasema . . . Nikasema, “Ilikuwa nini?”

²⁴ Kasema, “Loo, toka nje uangalie, Ndugu Branham, ni mvulana mdogo aliyeuawa. Kulikuwa na mwingine aliyeuawa pia, wanawazia, tayari wamempeleka hospitalini.”

²⁵ Nilisema, “Loo, sitaki kwenda.” Nikasema, “Ninawazia juu ya mvulana wangu mdogo, Billy Paul, wakati huo.” Alikuwa ni mtoto tu, nami nilikuwa sijamwona kwa miezi kadhaa. Na kama nyote mnajua, mama yake amekufa, nami nimekuwa mama na baba kwake, na hiyo ndiyo sababu tumeungana pamoja. Aliniomba kamwe nisimwache Billy, alipokuwa akifa, nami . . . Yeye ni—amekuwa rafiki yangu mpendwa tangu wakati huo.

²⁶ Na mimi—mimi—mimi sikutaka kumtazama huyo mtoto mdogo. Ingeleta tu... Angekuwa na karibu umri wa Billy wakati huo, kama umri wa miaka tisa, kumi. Na nyote mnakumbuka jinsi nilivyowaambia jinsi huyo mvulana angefanana: Alikuwa na moja ya hiyo mitindo ya kukata nywele kama farasi mkongwe na macho ya hudhurungi. Naye alikuwa maskini... amezivaa, zile tulizokuwa tukiziita katika siku zangu, “surukiuno,” kitu kama hicho, halafu so—soksi zake ndefu na mguu wake ungepondwa-pondwa katika soksi zake na ninii yake... Angeuawa katika ajali.

Vema, sikuenda, naye Bibi Isaacson alisema, “Ninaamini inakupasa kwenda kule.”

²⁷ Nikaenda kumwangualia huyo mvulana mdogo, nikaenda kule nao walikuwa wamemfunika uso kwa koti lake. Wakati nilipomwona maskini yule jamaa mdogo amelala pale, akiwa amepondwa-pondwa namna hiyo, nilininii tu—nilianza tu kulia. Nikageuka na kitu Fulani kikaweka mkono Wake juu yangu. Nilifikiri ilikuwa ni Ndugu Moore. Nikaangalia pande zote, na hapakuwa na mtu karibu nami, na mkono huo ulikuwa bado umewekwa begani mwangu. Vema, nikasema, “Ajabu hiyo.” Ndipo huo mkono ukaniacha.

²⁸ Sijui kama mnaamini, nyote mnaamini katika mambo ya kimbinguni au la, lakini lilitukia, vivyo hivyo tu. Kisha nikaanza kuondoka tena, nao ule mkono ukawekwa begani mwangu tena. Nikawazia, “Vema, sijui kile hili linachomaanisha. Labda ninapaswa kumwomba mtoto huyu mdogo.” Ndipo nikawazia, “Vema...”

²⁹ Nikaangalia nyuma tena, walikuwa wamekwisha kuufunika uso wake mdogo. Na kulikuwa na watu kama mia tatu waliosimama pale. Na nikaanza kuondoka, huo mkono ukanishikilia tu. Vema, nikasema... nikarudi nyuma, ndipo nikaanza kurudi kuelekea kwa yule mvulana mdogo, nao ule mkono ulikuwa sawa, ukaniacha. Vema, nilifanya hivyo mara mbili. Nami nikasema, “Hebu nimwone maskini yule mvulana tena.” Ndipo wakainua ninii... Bibi Isaacson akiongea kwa niaba yangu, kuyafasiri, nao wakainua ki—kitu hicho nipate kuona uso wake tena. Ndipo nikaangalia. Nikawazia, “Ajabu hiyo. Inaonekana kana kwamba nimemwona mvulana huyo.”

Vema, Daktari Manninen, alikuwa ndiye kiongozi wa Shirika la Wahudumu wa—wa Helsinki, na kwa hivyo mimi... Yeye alikuwa pamoja nami.

Nikasema, “Dk. Manninen, mvulana huyo mdogo a—amepata kuwa kwenye mstari wa maombi?”

³⁰ Akasema, “Sidhani.” Kasema, “Nitawauliza baadhi ya wachungaji wa hapa.” Nao walikuwa wamesimama pale. Hapana, walikuwa hawajawahi kumwona huyo mvulana mdogo, hawakumjua.

³¹ Nikasema, “Ajabu hii; inaonekana kama kwamba nimemwona huyu mvulana mdogo.” Nikaanza kuondoka tena, ndipo mkono huo ukawekwa begani mwangu tena. Nikatazama nyuma, nami nikawazia, “Kitu fulani ni cha kig- . . .”

³² Ndipo nikaona: maskini nywele zimekatwa mtindo wa farasi mzee, macho madogo ya hudhuri yametokeza, amelala chali, mguu mdogo kwenye soksi zake ambapo ilikuwa imepondwaponywa namna hiyo. Loo, alikuwa katika hali mbaya sana. Gari hilo lilimzungusha-zungusha tu namna *hiyo*, na gurudumu la nyuma baada ya kupoteza udhibiti, likamruska nje, naye alininii tu—alikanyaga ki—kichapuzi namna *hiyo*, nalo likaenda tu juu ya kilima. Mtu huyo kamwe hakuumia; walimtoa kwenye mabaki ya gari, naye alikuwa peke yake. Ndipo nikaangalia tena, na ku—kuangalia juu ya kile kilima. Na kulikuwa na hiyo misonobari iliyokuwa ikitokeza kilimani, viunga hivyo vya mwamba.

³³ Loo, jamani! Marafiki Wakristo, natumaini kwamba siku moja, ikiwa sio hapa, tutakuwa katika nchi nyingine, wakati hisia hiyo inayokuja kwako wakati unajua. Laiti ningalikuwa na hisia hiyo wakati wote. Iwapo ningeweza . . . Ni kitu fulani. Ni upendo; ni kama upendo wenye kilindi. Nami . . . Kama—kama shetani angalituma vishetani vyake vyote kutoka matesoni na kusimama pale pale kwenye maeneo hayo, ingekuwa . . . wasingaliweza kuondoa hisia hiyo hata kidogo. Ni jambo ambalo Mungu amesema litatukia nawe unaliona papa hapa liko mbele yako. Litatokea.

³⁴ Kwa hivyo nikasema, “Namjua mvulana huyo.” Naye Ndugu Moore na hao wengine wamesimama pale. Nikasema, “Angalia katika Biblia yako, Ndugu Lindsay, ukurasa wa kwanza usiopigwa chapa.” Mnajua, niliwaomba ninyi watu, wakati nilipopitia hapa, ilikuwa Portland wakati huo, kuandika kwenye ukurasa wa kwanza usiopigwa chapa wa Biblia yako. Nililiona kwenye garimoshi nikienda Florida. Nami nikasema, “Nililiandika hapo, ‘BWANA ASEMA HIVI, mvulana mdogo,’ nikaelezea umbo lake, ‘angefufuliwa kutoka kwa wafu.’”

Naye akatazama ukurasa wa kwanza usiopigwa chapa wa Biblia, ndipo Ndugu Moore akasema, “Huyo ndiye yule mvulana.”

³⁵ Nikasema, “Huyo ndiye.” Nikasema, “Sasa . . .” Nami nikawaambia watu wote kisha nikamwambia na Bibi Isaacson, nikasema, “Sasa, waambie, ‘Iweni tu na kicho.’” Nikasema, “Ikiwa mvulana huyu mdogo hatakuwa amesimama kwa miguu yake, akiwa hai, katika dakika tano kuanzia sasa, basi mnaweza kuniondosha Finland; mimi ni nabii wa uongo.” Mnaona? Nikasema, “Huyu mvulana mdogo atafufuka katoka kwa wafu sasa hivi,” amekufa kama dakika thelathini.

³⁶ Na kwa hiyo, walikuwa wakimngojea baba na mama, nami nilikuwa nikiwazia jinsi hapana shaka walijisikia, jinsi watakavyojisikia wakija, kumwona mvulana wao mdogo amepondwa-pondwa na amelala barabarani namna hiyo. Maskini ulimi mdogo ulikuwa ukining'inia, upande wa kinywa chake, damu ikitoka masikioni mwake, na kila kitu. Kwa hivyo, nikapiga magoti jinsi lile ono lilivyoonyesha, nikamwekea mikono maskini huyo mvulana, na mara tu nilipomwekea mikono, nikasema, "Baba wa Mbinguni, huko Marekani miaka miwili iliyopita, uliniahidia maisha ya mtoto huyu, kwamba atafufuka tena. Sasa, mauti hayawezi kumshikilia wakati ono hilo likizungumza." Nikasema, "Mauti, rudisha uhai wake katika Jina la Yesu Kristo."

Mvulana mdogo akaruka juu na kupiga mayowe...?... mwajua. Alikuwa tu wa kawaida na mwenye afya kadiri mtoto yeyote angaliweza kuwa.

³⁷ Sasa, nimeandikiwa hayo na mkuu wa jiji la Kuopio, Finland, katika somo langu la leo. Hiyo ni kweli. Liko kule limeandikwa halafu likatafsiriwa upande huo mwingine, jinsi ilivyokuwa. Kasema, "Ndugu Branham, sisi ni maskini nchini Finland. Hatuwezi kukupa chochote, kitu pekee tulicho nacho ni karatasi, kwa hivyo hiki hapa kitabu cha Kuopio na maoni kutoka kwangu." Nacho kina muhuri wao juu yake namna *hiyo*, wakati alipoandika huo ushuhuda mwenyewe.

³⁸ Mtu fulani aliniandikia kutoka Finland hapa si muda mrefu uliopita. Kasema, "Huo ulikuwa ni uongo." Naye alikuwa akitaka kuandika kitabu juu yake; ulikuwa ni uongo.

³⁹ Nami nikasema, "Endelea moja kwa moja, andika tu hicho kitabu. Ndipo nitachapisha ushuhuda huu wa meya wa jiji nyuma yake. Kwa hivyo sasa, wewe endelea tu na uandike chochote unachotaka."

⁴⁰ Je, tuna dakika moja tu, mbili, zaidi kwa kitu fulani? Nataka kumaliza hiyo. Usiku huo tulipoondoka Finland, hiyo...Tulikuwa tukienda mahali hapo; kulikuwa na wengi sana huko; ilibidi wawe na walinzi mtaani. Nami nilikuwa nikiingia chumbani, hapo, nilikuwa nikitembea; kulikuwa na karibu askari sita au saba karibu nami. Hao Wafini maskini walikuwa...si wazima kutosha kunyoa ndevu bado, wanaume wengine wote wazima walikuwa karibu wote wameuawa na Warusi. Na kwa hivyo, walikuwa wakinipeleka ndani.

⁴¹ Na ukizaliwa nchini Urusi, iwapo uko maili arobaini kutoka mahali ulipozaliwa, inakubidi kuwa na visa. Lakini usiruhusu mtu yeyote akwambie hakuna Wakristo katika Urusi; kuna mamilioni yao. Na kulikuwa na wale askari wa Urusi ambao... Hawawezi kutangaza vitu kama tulivyofanya, roki na upuuzi huo wote, huko juu...hakuna ila biashara na mambo ya uchumi

biashara kwenye—kwenye redio. Na hapa, hiyo ingeenda kote Urusi. Mimi. . .

⁴² Baron von Blomberg aliniambia muda si mrefu uliopita, jamaa mdogo ambaye walikuwa wamemtoa nyuma ya Pazia la Chuma, kasema, “Nimeshangaa, Ndugu Branham, kwamba huduma yako haijulikani Marekani kuliko vile ilivyo.” Inajulikana vizuri zaidi huko Urusi kuliko ilivyo hapa, ambapo ilikuwa nyuma ya Pazia la Chuma. Akasema, “Sisi sote tulisikia kwenye—kwenye redio, yule mvulana mdogo akifufuliwa kutoka kwa wafu kule juu.” Na sasa, hii. . . Hao wanajeshi wa Urusi waliosimama barabarani, walipiga saluti hiyo ya Kirusi wakati nilipopitia hapo. Nao wangesema. . . na mkalimani akaniambia wakati wakipita, kasema, “Walisema, ‘Tutampokea Mungu kama huyu.’” Bila shaka.

⁴³ Mnaona? Jambo ni kwamba, udhaifu wa kanisa ndio uliouiinua Ukomunisti; ulianguliwa kutoka kwenye yai la namna hiyo. Kama kanisa lilichukua pesa zote zilizomo nchini na kujenga madhabahu za dhahabu za dola milioni moja, na huku watu wanakufa kwa njaa barabarani? Mnaweza kuona ni kwa nini mambo kama hayo yatatokea. Lakini hebu mwanadamu yeyote aone jambo halisi la Mungu, ataliadini, iwapo ana kitu chochote ndani yake cha kuaminia.

Kwa hivyo alikuwa amesimama pale, naye akasema, “Tutampokea Mungu kama huyu, anayeweza kuwafufua wafu. Tunataka kujua kuhusu hilo.”

⁴⁴ Nami nitawaambia, wakati nikiwa kwenye somo hili, naweza kusema hivi: nimeona askari wa Kirusi wakiwakumbatia Wafini kiunoni mwao, mle ndani upande wa ndani ya jengo, na kukumbatiana na kupapasana, kama vile watu wa Skandinavia wanavyofanya, kukumbatiana na kupapasana. Chochote ambacho kitamfanya Mrusi kumkumbatia Mfini, na Mfini kumkumbatia Mrusi, kitamaliza vita milele. Hatuhitaji ma-U.N.; tunamhitaji Yesu Kristo. Hicho ndicho ulimwengu unachohitaji. Mnaona?

⁴⁵ Nilipokuwa nikiingia usiku huo, kulikuwa na msichana mdogo aliyetoka nje. Wewe ambaye umeisoma hiyo hadithi; wewe. . . Ndugu Gordon, kamwe hakuiandika kwa utondoti; kwa namna fulani aliitaja tu. Alikuwa ametoka kwenye bwani la wanawake, kama ilivyokuwa. Basi tulipoanza kutembea huku na wale askari, ndipo yule msichana mdogo, alipotoka nje, alikuwa na mguu mmoja uliokuwa mfupi hivi kuliko huo mwingine. Halafu amejizungushia m—mkanda mkubwa, na ga—ga—gango lililoshuka chini, la kujitengenezea, namna *hiyo*, naye alikuwa na magongo mawili. Alikuwa na kamba mwishoni mwa kidole chake cha miguu iliyopitia begani mwake na kufungiwa hapa nyuma ya mshipi huu. Basi alipoanza kutembea, alikuwa, aliweka magango yake nje, au, magongo nje, kisha akachukua

maskini bega lake na kuuinua huo mguu mdogo juu na kuuweka namna hiyo, kisha anapiga hatua yake. Na kwa hiyo, akaniona.

Nao walikuwa wamewaonya, mnajua.

⁴⁶ Ninapenda watoto, nami ningeenda mtaani nikiwa na maskini pesa hizo za Kifini na kununua lundo kubwa la peremende hizo, unajua. Na ndugu, ningekuwa nikiwapa watoto. Nilikuwa na mlolongo kutoka hapa, mijengo miwili ya mji, walionifuata kila mahali, maana na—nawapenda watoto.

⁴⁷ Na kwa hivyo basi nikamtazama, akakiinamisha maskini kichwa chake namna *hiyo*; alihofu alikuwa amefanya kitu kibaya. Nami nikamtazama mtoto huyo na nikaanza, kuondoka, ndipo kitu Fulani kikasema, “Ongea na mtoto huyo; anataka kuzungumza nawe.”

⁴⁸ Nikasimama. Nao hao askari wakaendelea . . . Hawakuweza kuzungumza Kiingereza, kwa hivyo wakazidi kusonga mbele. Ningeweza kuwasikia wakiimba, *Amini Tu*. Na kwa hivyo nilipoanza kufanya hivyo, askari hao waliosimama tu pale. Nami nikasema, “Hebu kidogo tu hapa.” Hao askari wengine wakaangalia nyuma. Nami nikasema, “Hebu kidogo.” Mnaona?

⁴⁹ Na kwa hivyo, msichana huyo mdogo, nilimwangalia, ndipo nikasema, “Njoo hapa, kipenzi.” Asingeweza kuelewa; alionekana kuwa na umri wa karibu miaka tisa, kumi. Ndipo nikasema, “Njoo hapa, kipenzi.” Naye akakiinamisha maskini kichwa chake; maana hakuelewa niliyokuwa nikisema. Na mimi—mimi . . . Akaniangalia tena, na kuinamisha maskini kichwa chake upesi sana, kama mtoto. Na nikamwashiria *hivyo*, “Njoo hapa.” Naye akanyosha magongo yake madogo, akainua mguu huo juu na huyu hapa anakuja. Nikasimama tu kimya, nao wale askari wakasimama pale wakitazama tu kilichokuwa kikiendelea.

⁵⁰ Akafika karibu sana nami, mahali nilipokuwa, namna *hiyo*. Akasimama tu, akakiinamisha maskini kichwa chake, na sketi yake ndogo chakavu ikining’inia chini, maskini nywele zake juu ya uso wake. Niligundua baadaye alikuwa yatima wa vita wa Kifini; mama na baba yake waliuawa. Alikuwa akiishi katika hema. Na—nami nikatazama, naye akaniangalia namna *hiyo*. Aliniangalia, na machozi makubwa yakidondoka kutoka kwenye maskini macho yake, yakitiririka usoni mwake namna *hiyo*.

⁵¹ Akanyosha mkono akalishika koti langu, na kunibusu tu kwenye mfuko wa koti langu; kisha akavuta sketi yake ndogo *hivi*, maskini ile sketi chakavu. Akasema, “*Kiitos*.” Hiyo inamaanisha “asante.” Moyo wangu ulikuwa juu tu kinywani mwangu; unajua jinsi unavyohisi hivyo; mtoto huyo mdogo. Nami nikatazama nje hivi, ndipo nikamwona amesimama pale nje bila magongo wala magango, akimsifu tu Mungu.

⁵² Nikasema... Ninaamini kama ningelikuwa mnaifiki mkubwa zaidi ulimwenguni, Mungu angeiheshimu imani ya mtoto huyo. Hakika ataiheshimu; angeiheshimu.

Tena nikasema, “Kipenzi, uh, loo, nawezaje kukuambia?” Ni—nikasema, “Umepona, kipenzi. Mungu amekuponya.”

“Jeesus,” akasema, “*Kiitos, Jeesus.*” Hiyo ni “Asante, Yesu.”

Nikasema, “Anakufanya...”

Sikuweza kujua maneno mengine, mnaona, nikasema, “Amekuponya. Kiitos Yesu akuponya.” Hangeweza kuelewa hilo. Na halafu wao...

Huyu hapa Ndugu Baxter anakuja mlangoni, naye akasema, “Haya njoo, njoo.”

Nami ni—nikawazia, “Vema, Mungu atamjulisha siku moja, kwa hivyo nikaingia tu. Angekuwa, angepata afya, apone.”

⁵³ Kwa hiyo nikaingia, na tulikuwa na mstari mrefu sana wa maombi. Mliiona, ile picha kwenye kitabu cha malundo makubwa ya magongo na kadhalika, yamelundikana tu kunizunguka namna *hiyo*. Mara tu hiyo...

⁵⁴ Nini kilitokea usiku huo? Kulikuwa na yapata watu wanane ama kumi waliokuja jukwaani. Na halafu, kulikuwa na mwa—mwanamke kama wa Laplandi ameketi kule nyuma, alikuwa na mtoto mwenye makengeza; alikuwa amemlaza sakafuni. Roho Mtakatifu akazunguka, wala sikuweza kumpata. Nikawazia, “Bwana, nisingeweza kutamka jina hilo; hebu nitaje tahajia zake.”

⁵⁵ Na nikaanza kutaja tahajia za jina lake, nikamwambia yeye ni nani, yote kumhusu, namna *hiyo*, na shida ya mtoto wake mchanga. “Mchukue ukamwangelie,” akasema; akitaja tahajia zake, sasa, kwamba alikuwa... Na jinsi alivyolielewa, sijui mimi. Alimnyakua mtoto huyo na kumuangalia, nayo macho yake sawa kabisa kama yawezavyo kuwa. Karibu aninii... Karibu ashikwe na kifafa, huku na huku tu sakafuni akipiga mayowe, ambapo maelfu ya watu...

⁵⁶ Halafu Howard, kama tu Billy afanyavyo sasa, ndugu yangu, aliponigusa ubavuni... Nilikuwa karibu sijifahamu chini ya maono hayo. Akanigusa namna *hiyo*, “Wakati wa kuondoka.” [Ndugu Branham anajipapasa ubavuni—Mh.]

Nikaanza kuondoka, kitu Fulani kikasema, “Ngoja kidogo; waite wengine.”

Nikasema, “Hebu kidogo, Howard.” Nikasema, “Usinichukue sasa.”

Alisema, “Kwa nini?”

Nikasema, “Hebu tuite watu wengine watano.” Nikamwambia, Bibi Isaacson, nikasema, “Ita kwa Kifini ninii—ninii... namba unazopaswa kuita.”

57 Basi akaita nyingine. Na kwa neema ya Mungu, kutoka humo chumbani, maskini msichana huyo alikuwa ndiye aliyefuata na kadi ya maombi; jinsi Mungu katika ukuu Wake.

58 Enyi marafiki, ninawaambia: jambo kubwa zaidi ambalo nimewahi kuona maishani mwangu ni kujisalimisha tu kwa Mungu na kutembea katika Roho, mnaona, siku tu baada ya siku, jinsi atakavyokuongoza na kufanya mambo.

59 Ndipo nilipomwona msichana huyu mdogo akija, niliwazia, “Bwana asifiwe.” Walimleta jukwaani, wakamsaidia kusimama. Ndipo mabawabu wawili au watatu wakamleta kwangu, wakambeba, kisha wakamketisha. Nilisema, “Sasa, Bibi Isaacson, angalia hili.” Nikasema, “Sasa, sema tu maneno ninayosema.”

Naye akasema, “Nitasema.”

60 Nilisema, “Kipenzi, Yesu Kristo aliheshimu imani yako huko nje wakati ulipobusu mfuko wangu muda mfupi uliopita. Ulikuwa unatoa heshima kwa vitu ambavyo uliwazia ni vya Mungu.” Nikasema, “Mungu amekuponya. Sasa, nenda pale uketi uwaache baadhi ya wahudumu au wengine wakutoe hayo magango. Nawe uweke mkono wako kwenye nyonga yako *hivi*.” Basi nikampa kitu cha kufanya ili kudumisha ujasiri wake, mnaona?

61 Kwa hivyo nikasema, “Unapokuja... Wakati uko... Wakiyatoa hayo magango, na hiyo kulabu kubwa ya chuma kutoka chini ya mguu wako hapa, wakikiondoa hicho, uteremshe mkono wako kwenye mguu wako kadiri unavyowazia hilo gango lilivyo, ufupi wa mguu wako.”

62 Na kwa hivyo nikasema, “Leteni mtu mwingine, sasa.” Nao walileta wa pili. Hao wahudumu wakampeleka kule. Bibi Isaacson kuitafsiri, nao wakampeleka kule na kuanza kukifungua kitu hicho.

63 Kwa hivyo, muda si muda mwajua, nikamsikia akipiga mayowe. Huyu hapa anakuja jukwaani, miguu yote miwili kawaida kabisa, magongo hayo juu ya kichwa chake, akipiga kelele na mayowe. Loo, jamani. Ilikuwa ni jambo moja baada ya lingine, baada ya lingine, baada ya lingine.

64 Nikaenda nyumbani usiku huo, nikatazama upande ule mwingine, nikiwaona wale Wafini wakitembea kule, mikono yao juu hewani, wakimsifu Mungu. Hapo ndipo Malaika alipoonekana juu ya yule mvulana mwingine mdogo. Someni hadithi ya hayo katika—katika kile kitabu. Na jinsi ambavyo yule mvulana mdogo, akiwa amelala hapo akifa, madaktari walikuwa wamemkatia tamaa, aliponywa kesho yake jioni jinsi tu Roho Mtakatifu alivyosema ataponywa. Ndipo akaondoka na akawa mzima, anaishi leo; ningali ninapata barua kutoka kwao, kwamba Bwana aliwaponya. Angali ni Yesu Kristo.

⁶⁵ Ni tamu: Asante, dada yangu mdogo, kwa zaka hii. Kama mhudumu, ninapaswa kupokea zaka. Kwa hiyo, nakushukuru sana, maskini msichana kipenzi changu. Mungu na akubariki daima. Wala usiache mama yako akuambie wewe ni mnene. Wewe si mnene. Unaona? Vema. Alisema humu ndani, sikusoma hayo; alisema, “Mama anasema mimi ni mnene, lakini sivyo nilivyo.” Wala mimi siamini u mnene. Kwa hivyo, ikiwa uko hivyo, Mungu na akupe shauku ya moyo wako, kipenzi, ndilo ombi langu, endapo linamaanisha chochote kwa Mungu kwako.

⁶⁶ Sasa, usiku wa leo nilitaka kutoa tukio lililotokea. Basi kwanza, nataka kusoma Ne—Neno. Sasa, kesho alasiri. . . (Ibada zitaanza saa ngapi, Ndugu? Saa nane u nusu.) Sasa, kesho saa saba u nusu, wote wanaotaka kuninii. . . kuja kwenye mstari wa maombi kuombewa, tutakuwa tukisambaza kadi za maombi, tukileta kundi zima kama tulivyofanya jana usiku. Hivyo ndivyo nafikiri huduma yangu itaanza na kuendelea kutoka jana usiku. Ninyi nyote mnaotaka kadi ya maombi njoni saa saba u nusu kesho alasiri, si baada ya—ya. . . iweni hapa kabla ya saa nane ama saa nane na robo, kwa sababu labda kadi zote zitakuwa zimesambazwa kufikia wakati huo, wala haitakatiza mkutano wote.

⁶⁷ Sasa, kama baadhi ya jumbe zingine nilipokuwa nikihubiri, ikiwa unazitaka, wale wavulana wanazo hapa, Ndugu Goad na Ndugu Mercier. Wako wapi, Gene? Kibandani nyuma ya jengo, wana santuri na kanda. Wavulana hawa, hizo ni. . . hizo ni zao, na wao ni. . . watafurahi kukupa. Na nimeitafuta katika mauzo yao na kadhalika.

⁶⁸ Niliwaambia hadithi jinsi ambavyo hawa wavulana walivyounganika nami jana usiku. Nami nilimtuma mhudumu muda si mrefu uliopita kununua kanda. Alinitoza dola tisa kwake. Nami nikawaangalia hawa wavulana, nami nafikiri ni kama dola mbili na nusu, au, kitu kama hicho; wanapata karibu senti thelathini na tano, arobaini, labda, senti hamsini kwa kanda, huku wakinunua kanda iliyo bora sana, Kanda ya Scotch, na kutengeneza zilizo bora sana. Wakiweka bei kubwa juu yazo, ningewaambia hivi sasa: “Hakuna kuuza kanda tena!” Hapana, bwana.

⁶⁹ Sasa, inawabidi kupata kitu kwa kazi yao, maana wanavunja kanda nyingi, na kila kitu, tena i—inawapasa kupata riziki. Mmoja wao ni mtu aliyeoa, na kwa hiyo sisi. . . Hawana budi kupata riziki, nao wana haki ya kupata faida kidogo kwazo. Na halafu wakati mwingine, huharibika na kuvunjika, nao wanazituma huko nje wala hawalipwi, nanyi, mnajua jinsi mambo yanavyoendelea. Kama tu vitabu vyetu huko nyuma: Ninanunua hivyo kutoka kwa *Sauti ya Uponyaji* kwa kupunguziwa asilimia arobaini. Na, huku ikitubidi kulipa kwa ajili ya kuviuza, na gharama ya kuvishughulikia. . .

Nami nimesema sikuzote, “Mtu yeyote akitaka kitabu...” Nimewapa hao wavulana agizo wakati wote:

Mtu yeyote akitaka kitabu, na mzee maskini apande aje, na kuingiza mkono mfukoni, “Vinauzwaje?”

“Vema, vinagharimu senti sabini na tano,” au, chochote wao... dola, au, bei yoyote ile.

Naye akasema, yeye, “nina senti sitini.”

Mwambie, “Baba, chukua kitabu uende zako; sahau kuhusu hilo.”

⁷⁰ Mnaona? Acha kiende. Kwa njia hiyo, vitabu hata havijitegemei. Inabidi kanisa linisaidie kuvigharamia vitabu. Sisi... Kufikia wakati tunapovilipia, na kuvichapisha, na—na kuharibika, na kuraruka, na chochote kile juu yavyo, na vile vinavyotubidi kutoa bure na kadhalika, mbona, hivyo—hivyo havininii... havijite... havijitegemei. Na kwa hiyo basi, hatuna chochote kinachotupatia faida. Kila kitu tufanyacho...

⁷¹ Na mimi mwenyewe: Sadaka yangu ya upendo huenda kwenye huduma ya kimishenari. Siioni. Inakwenda kwa jambo zuri. Ninapata dola mia moja kwa wiki kutoka kwa kanisa langu, iwe Marekani, nje ya Marekani, kokote kule, ninapata dola elfu tano mia mbili kwa mwaka. Hiyo ndiyo riziki yangu, nasi inatubidi kujinyima, tukiwa na familia kubwa kama niliyo nayo. Nami inanibidi kuishi katika nyumba ya mchungaji wa kanisa.

⁷² Wala kamwe hatuji hapa kwa ajili ya pesa; hiyo siyo nia yetu. Sababu pekee tunayoruhusu... tunayonunua vitabu na kuviuza tena, na kuuza kanda na hayo, ni kwa sababu tunafikiria kuwa itaiendeleza huduma ya Yesu Kristo. Hakuna pesa ndani yake hata kidogo. Lakini sitaruhusu vitabu au kanda au chochote kile kuuzwa siku ya Sabato. Hiyo ni kesho. Hatutaviuza Jumapili; hatujawahi kuviuza, wala kamwe hatukusudii kufanya hivyo. Na kwa hivyo ikiwa unataka baadhi ya hivyo vitabu, baadhi ya kanda au santuri, zitakuwa nyuma ya hili jengo usiku wa leo.

⁷³ Na kama ukikipata, na hufikirii... Ikiwa huna pesa zozote, ni chako hata hivyo. Ukikipata, hakina thamani ya hizo senti hamsini, ama chochote ulichokilipia, kirudishe moja kwa moja, ama ukitupe kisha utwambie, ama umpe mtu mwingine. Mpe mtu mwingine, kisha utume habari na utuambie hakikustahili hizo; utarejeshewa hizo pesa. Kwa hivyo hatutaki chochote ambacho... Gharama yoyote, kitu kama hicho hata kidogo. Ni bure.

⁷⁴ Lakini sa—sadaka ya upendo ni kwa ajili ya nchi za kigeni. Siipokei mimi mwenyewe; inachukuliwa na katibu wangu wa nje; inahesabiwa na wahudumu, anapewa, anaiweka benki. Basi ninapokwenda ng'ambo na kadhalika, inanisaidia katika nchi za kigeni kuleta ujumbe uu huu wa ukombozi kwa watu ambao

hawajui hata mkono wa kulia na wa kushoto ni upi. Huko ndiko inakoenda. Sijui kamwe, hata, sadaka ni ngapi, isipokuwa mtu fulani aniambie. Nitakapofika nyumbani, nitakuwa nimeondoka mwezi mzima, kwa hivyo nitapata dola mia nne nitakaporudi nyumbani kulipa madeni yangu na kadhalika. Sasa, hivyo ndivyo tunavyoishi, ili mweze kuelewa kuwa hatuna ninii yoyote. . . la, la. . . hatuji kwa ajili ya pesa, au kitu kama hicho. Na kile tulicho nacho, nataka kukiweka wazi kabisa mpate kukiulewa.

⁷⁵ Sasa, usiku wa leo kab-. . . Ninataka kuchukua somo dogo, ikiwa yanipasa kuliita hivyo, kulizungumzia kwa muda mfupi. Kabla hatujalikaribia, na tunamishe vichwa vyetu, kwa muda mfupi tu, kwa ajili ya maombi.

⁷⁶ Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kutoka kwenye vilindi hasa vya mioyo yetu. Jinsi ujuzi, Bwana, nimekuona ukifanya katika mikutano yangu midogo, sembuse wale watu mashuhuri walio hudumani, kama vile Ndugu yetu Roberts, na Tommy Osborn, na wengineo. Nimekuona ukifanya ya kutosha katika ibada zangu kuandika Biblia nyingi za mambo makubwa, ya kuwafufua wafu. Ukawajalia madaktari watie saini taarifa zake. Kuwafanya vipofu, viziwi, bubu; kutabiri, kusema yale hasa, kuyaona yakitokea kila wakati sawa kabisa. Wewe ni Mungu, nasi tunajua kwamba Wewe ni Mungu.

⁷⁷ Tafadhali, Baba, kukiweko miongoni mwetu usiku wa leo, mtu ambaye haamini, jalia jambo fulani lifanyike au kusemwa usiku wa leo, litakalomfanya mwanamume au mwanamke huyo kusalimisha kutokuamini kwao Kwako na kulibadilisha kwa Roho halisi wa imani kutoka kwa Mungu, Roho Mtakatifu. Lijalie, Bwana. Uko tayari kuuondoa uovu wao na kuwapa mema. Loo, Wewe ni mwema sana, Baba; tunakupenda kwa ajili ya hilo.

⁷⁸ Tunaomba kwamba utawavuvia wahudumu Wako kila mahali. Jalia wawe mienge inayowaka kufikia saa hii ya giza tunayoishi, tunapoona huo unaoitwa ustaarabu ukizima Nuru yenyewe ya Mungu, kama inawezekana. Lakini bado, mwenge huo utawaka moyoni mwa watu mpaka Yesu atakapokuja. Baba, ongeza zaidi kwenye safu usiku wa leo, tunaomba. Waponye wagonjwa wote, wote wanaoteseka, tunaomba kwamba neema na rehema Zako zitatulia juu yao. Wape Uzima wa Milele katika ulimwengu ujao, na uwape afya njema katika ulimwengu huu. Kwa maana imeandikwa katika Biblia, "Ningependa juu ya mambo yote, uwe na afya njema."

⁷⁹ Yavuvie makanisa kote katika hili bonde na kila mahali ambayo—ambayo yamewakilishwa katika uamsho huu mkubwa, wa Roho Mtakatifu, ambao umeenea ulimwenguni. Tunaomba, Baba, kwamba utaufufua tena katika njia kuu. Jalia uanze hapa Oregon tena, uamsho mkuu katika kila kanisa.

⁸⁰ Kesho, Sabato, makanisa na yajae, wahudumu na washike moto, na nafsi ziingizwe ndani, wengi na waje wakikiri dhambi zao na kuhitaji ubatizo wa maji. Lijalie, Baba. Na Wewe umjaze kila mmoja kwa Roho Mtakatifu, anayefuata maagizo Yako, kama tulivyofundisha hivi majuzi usiku. Ninaomba, Baba, kwamba utawajulisha kuwa ahadi hiyo ni kwa kila kizazi, na “kila atakaye; wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hivyo ndivyo maagizo Yako yalivyosema; tunaamini kila Neno lake. Ninaomba, Baba, kwamba utamjalia kila mtu hii.

Tusamehe dhambi yetu. Chukua ibada mikononi Mwako na ujipatie Mwenyewe utukufu, katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

⁸¹ Sasa, ningependa kusoma mstari mmoja tu kutoka kwenye mlango wa 4 na kifungu cha 17 cha Mathayo Mtakatifu:

Tangu wakati huo Yesu alianza . . .hubiri, na kusema, ufalme . . .Tubuni: kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.

⁸² Sasa, nataka kuchukua somo, hayo maneno matatu ya kwanza: *Tangu Wakati Huo*. Sasa, kunao wote hapa wanaoweza kukumbuka hata wakati *fulani-fulani*. “Tangu wakati huo,” tunasema. Kama vile maskini mvulana mdogo, msichana mdogo, tunaweza kusema tulikuwa tukifanya jambo *fulani* na *kitu fulani* kikatukia, na “tangu wakati huo” mambo yakatubadilikia.

⁸³ Nasi tunaweza kwenda, usiku wa leo, mjini, hapa, na kumpata mwanamke aliye duni sana na mtovu wa uadilifu anayetembea mitaani mwa maskini mji wenu wa kupendeza, hapa bondeni. Nami ningeketi chini karibu naye, na ningesema, “Mama, ningetaka unisimulie hadithi yako.”

⁸⁴ Na angeanza; huenda akasema kitu kama hiki: “Ndugu Branham, kulikuwako na siku nilipokuwa safi kama yungiyungi. Nami ningeweza kuinua kichwa changu kati ya watu wa hadhi maarufu; na ningeweza kwenda kanisani, na kujisikia vizuri tu. Lakini ukaja wakati ambapo usiku mmoja nilikuwa nje na mvulana fulani, na akaiongezea Ko—Koka yangu kitu fulani, na tangu wakati huo . . .”

⁸⁵ Au huenda ikawa kwamba rafiki mwingine wa kike ambaye hakuwa mwaminio, ambaye aliambatana naye na kumshawishi waende kwenye densi fulani. Ndipo akajikuta mikononi mwa mvulana fulani, na tangu wakati huo. Sikuzote ni kukumbuka kuanzia wakati fulani.

⁸⁶ Au naweza kwenda nje hapa katika jiji lenu usiku wa leo, na kumpata mlevi sugu mbaya sana mliye naye. Nami ningeketi chini kando ya mtu huyo, kijana au mzee, nami ningemwambia, “Rafiki, ningependa kukuuliza kitu: Kwa nini kuyatupa maisha yako hivi? Ni nini kinachokufanya unywe

pombe na kufanya vile ufanyavyo? wakati ungeweza kuwa m—mfanyakazi mkubwa hapa mjini. Ungeweza kuwa mfanyakazi katika kanisa fulani, au ungeweza kuwa mume wa kweli kwa mwanamke fulani, baba kwa watoto fulani;” au, mwanamke fulani mlevi ambaye angeweza kuwa ma—mama halisi kwa watoto fulani, mke mwema, mwenye upendo kwa mume fulani.

⁸⁷ Na wangeanza hivi, na kusema, “Kweli, tangu... Wakati mmoja nilikuwa mpinga pombe. Nilikuwa na mama na baba wazuri ambao walifundisha dhidi ya kunywa pombe. Ndipo wakati mmoja niliingia kwenye ushirika na mvulana fulani ambaye alikuwa maarufu sana miongoni mwa wasichana, nami ni—ni—nilitaka kuwa maarufu pia, kwa hivyo nikafikiria nijiunge na njia zake. Basi nikaenda kinyume na mafundisho ya mama na baba yangu. Naye akanishawishi, ‘Usiku wa leo ukitaka kuwa na wakati mzuri, ukitaka kuchangamka.’ Basi nikanywa kinywaji changu cha kwanza, na tangu wakati huo...”

⁸⁸ Hivyo ndivyo ianzavyo. Hapa wakati fulani uliopita huko New York, Dk. Berg, yeye ni mchungaji sasa kwenye maskani ya Dada Brown, Maskani ya Bethania, katika Jiji la New York, moja ya vituo vya kale vya Pentekoste, moja ya zamani sana ulimwenguni; nadhani ndugu zetu wanawajua vizuri.

⁸⁹ Basi huko, nilipokuwa huko, nilikutana na Sophia, mwanamke mfua nguo, yule mwanamke wa Uswidi aliyeenda na kufanya kazi naye kwenye mtaa wa walevi sugu. Nililazimika kulala zaidi ya siku mbili kudungwa sindano ya homa ya manjano; nilifikiri ningeingia Afrika bila kudungwa, lakini hata wasingeniruhusu kupita, au, kuingia kwenye ndege. Na ilibidi ningoje siku mbili kwenda kwenye uwanja wa Jeshi la Wanamaji kudungwa sindano ya homa ya manjano.

Naye Ndugu Berg akasema, “Ungependa kufanya nini?”

Nikasema, “Ningependa kuutembelea mtaa wa walevi sugu.”

Kasema, “Sawa, tutashuka twende.” Kasema, “Ninazo misheni kadhaa kule chini.”

⁹⁰ Nasi tukashuka kule, na kama mimi... Nadhani lingekuwa ni jambo zuri kwa mwanamume yeyote kumpeleka mwanawe kwenye mtaa wa walevi sugu na kumwacha ajionee. Nafikiri ikiwa uliwahi kuwa Ufaransa, mpeleke binti yako Pigalle; umwache aone jinsi maisha ya mwanadamu yanavyoweza kudhalilika.

Kwa hiyo niliposhuka kwenda... kwenye huo mtaa wa walevi sugu, wanaume wamelala hawajiwezi, nzi wakipuliza usoni mwao kutokana na matapiko, na loo, walevi sugu wa kasumba, walevi sugu wa pombe.

⁹¹ Ndipo nikasema, “Loo, Ndugu Berg,” nikasema, “labda wanaume hawa hapa walilelewa katika nyumba ambazo—

ambazo hawajali wafanyayo; waliachiliwa huru tu kukimbia mitaani.”

⁹² Aliweka mkono wake begani mwangu, akasema, “Utashangaa.” Akasema, “Papa hapa katika misheni hapa tunakokwenda, tuliwatoa mia moja na themanini waliokufia huko mwaka jana. Walioondolewa mitaani, kuwalisha na kadhalika, na mwishowe wakafa; hakuna tumaini kwao nje ya Kristo.”

Halafu, tiba, wamevuka mpaka hawatibiki. Akasema, “Hapa, mtu huyu hapa.” Kasema, “Namjua. Mwinue.”

Basi nikamwendea, nikasema, “Bwana, naweza kuongea nawe?”

Akasema, “Vema, huenda asiweze kuongea.”

⁹³ Loo, kamwe siwezi kusema hali aliyokuwa nayo mtu huyo. Alikuwa amefika mahali nguo zake kutoka kiunoni kwenda chini zilikuwa katika hali mbaya kabisa, zimelowa kila mahali. Naye alikuwa tu katika—katika hali mbaya mno, ananuka. Basi nikasema, “Bwana, naweza kuongea na wewe?”

⁹⁴ Ndipo Ndugu Berg akamtikisa. Mimi...Akainuka. Akasema, “Mimi ni Ndugu Berg.” Vema, hakujua chochote kuhusu Ndugu Berg. Bado alikuwa kwenye ulevi.

Nikasema, “Ningependa kukuuliza swali.” Nikasema, “Ulilelewa katika makazi ya aina gani?”

Akasema, “Je, utanipa pesa za kutosha kinywaji?”

⁹⁵ Nikasema, “Mimi ni mhudumu wa Injili. Nisingempa mtu pesa za Bwana anywe.” Nikasema, “Mimi...Fedha nilizo nazo zinatoka kwa watoto wa Mungu, na zinafaa kutumika kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nitakwambia nitakachofanya: nitakununulia sandwichi; nitakununulia chakula chako cha jioni au...ikiwa utaenda nami. Lakini ningependa tu, kama mhudumu, kukuuliza.”

Akasema, “Samahani, Kasisi.”

Nami nikasema, “Kweli, ulipataje kuwa hivi?”

Akasema, “Bwana, nina shaka kama utaamini hadithi yangu.”

“Vema,” nikasema, “Ninakuchukua kama mtu wa heshima. Ni—nitaamini hadithi yako, niambie; niambie kutoka moyoni mwako.”

Akasema, “Bwana,” akasema, “Nililelewa katika nyumba ya Kikristo.”

Nami nikasema, “Halafu ukatumbukia katika haya?”

⁹⁶ Akasema, “Naam, bwana.” Kasema, “Nilikuwa na familia ya kupendeza sana: watoto watatu, wavulana wawili na msichana, na mke mzuri sana aliyewahi kuishi.” Ndipo machozi yake

makubwa yakaanza kutiririka kupitia maskini ndevu zake, zenye mvi. Akasema, “Nilikuwa rais wa benki hii hapa kwenye kona *fulani*.”

Nikasema, “Kweli?”

Akasema, “Nenda kwenye benki ukawaulize.”

Naye... Nikasema, “Vema, ni nini kilisababisha ufanye hivi?”

⁹⁷ Akasema, “Bwana, kasisi bwana,” akasema, “jioni moja nilikuja nyumbani na kulikuwa na barua ya ‘Mpendwa John’ imewekwa mezani. Mke wangu alikuwa ameniacha.” Akasema, “Na mimi—mimi kamwe sikunywa pombe, ndipo bali nikawazia, ‘Sina budi kufanya kitu, la sivyo nitachukua bastola na kuzilipua bongo zangu.’ Ndipo nikaanza kunywa, nami huyu hapa.”

Nikawazia, “Mungu aturehemu.” Mnaona?

Kwenye... “Tangu wakati huo...” Hilo ndilo lililoyasababisha. Sikuzote tunaweza kukumbuka tangu wakati fulani.

⁹⁸ Basi kama vijana wawili wanaofunga ndoa. Loo, ni wa kupendeza kadiri wawezavyo kuwa. Muda si muda mwajua, ningemwendea mwanamke huyu aliyeiacha familia yake, na ningesema, “Mama, ni kitu gani kilikufanya uiache familia yako? Ulikuwa na mume mzuri.”

⁹⁹ “Loo,” angeniambia, angesema, “Ndugu Branham, mimi—mimi—mimi nilikuwa safi kama umande kutoka mbinguni. Niliolewa na mume wangu na nikamjia kama mwanamke mwadilifu. Naye alikuwa mtu mzuri; alifanya kazi na kutoa jasho na kunitunza. Na watoto wangeweza, mvulana wangu mpendwa, wakati alipozaliwa, ninaweza kumwona mpenzi wangu sasa amembeba maskini mvulana huyo mgongoni mwake, wamebebana huku na huku sakafuni. Na loo, laiti ningaliweza kuyarudia tena.”

Ningesema “Vema, nini kilitokea?”

¹⁰⁰ Angesema kitu kama hiki: “Vema, ilikuwa sawa. Ndipo siku moja, mchuuzi mwenye nywele nzuri za mawimbi-wimbi, na macho makubwa ya hudhurungi, alibisha mlango, na tangu wakati huo...” Unaona? Hivyo ndivyo inavyoanza; unaukumbuka wakati. Huo ni mwanzo wake tu.

¹⁰¹ Kamwe usifikiri kwamba dhambi iko mtaani, siku zote kwenye hali duni; dhambi imevalishwa kwelikweli na inapendeza. Hakika inavutia. Daima nimesema, “Shetani huvaa suti rasmi, na kofia maalum, na hubeba bakora mkononi mwake.” Mwangelie huyo mjanja anayeteleza. Hiyo ni kweli kabisa. Shetani sio mpumbavu, unajua. Yeye—yeye—yeye anajua kuvalia nadhifu; anaifanya ya kupendeza, mnaona?

¹⁰² Na sio kila wakati mzee Charlie Barleycorn huko nje na kofia yake iliyoinama; wakati mwingine huo ni moyo mwaminifu kweli. Kama angalikuwa na mwa—mwanzo mzuri ama chochote kile cha kumsaidia safarini, angeishia vizuri; bali si kila mara. Nimeona wakati mwingi, nami nimewaendea watu wenye matambara wawezavyo kuwa; ninawaangalia, nami nina njia ya Mungu ya kujua ni nani anayenipenda na ni nani hanipendi. Mnajua hivyo.

¹⁰³ Kwa hiyo, namwona mtu mchafu sana na kadhalika; afadhali niwe naye mara nyingi, kuliko mtu aliyevalia nadhifu pamoja na, labda, ukosi uliopinduliwa, na kunipapasa mgongoni, anasema, “Loo, Ndugu Branham, tuko pamoja nawe.” Na kujua papo hapo anadanganya. Mnaona, mnaona? Jambo ndilo hilo. Sina haja na mwongo. Jamani, unaweza kujificha kutoka kwa mwizi, lakini huwezi kujificha kwa mwongo. Kwa hiyo, hiyo—hiyo ni kweli.

¹⁰⁴ Lakini tunapofikia viwango hivyo, “Tangu wakati huo. . .” Basi Mwaka Mpya umefika. Ninyi nyote mnatoka nje na kuandika azimio. “Leo usiku, mke wangu, nitakupa ahadi. Nitafungua ukurasa mpya, nami si—sitakunywa pombe tena.”

¹⁰⁵ Naye huyo mwanamke alivuta sigara nyingi sana, hata hawezi kumnyonyesha mtoto wake tena, atampa sumu ya nikotini, amuue; na ataacha kuvuta sigara siku ya Mwaka Mpya. Mlevi ataacha kunywa pombe kwenye siku ya Mwaka Mpya; mtovu wa uadilifu ataacha uasherati wao siku ya Mwaka Mpya; kadhalika namna hiyo. Unafanya nini? Unafungua tu ukurasa mpya ukaufunge kesho yake tena. Unaona? Wewe. . .Ni. . . Hukuanza vizuri. Mambo haya yote ni mazuri; sina chochote dhidi yake. Lakini kuna. . .

¹⁰⁶ Ni kama tu katika vita. . .baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, wengi wenu ninyi watu wa makamu, na wa yapata rika yangu, nadhani nilikuwa na miaka minane au tisa wakati vita vilipoisha. Nami nakumbuka wakati walipotangaza vita: 1914, nilikuwa mtoto mchanga wa kiume nikiwa nimeketi kwenye mkokoteni wa springi. Baba yangu alikuwa na gunia la maharagwe; hayo ndiyo tuliyokula, maharagwe na ugali wa mahindi: tungali tunayapenda. Na kwa hivyo, wao. . .Baba alikuwa akizungumza habari za vita, na huenda ikabidi aende vitani.

Nilisema, “Kama jamaa hao wakija kukutafuta, nitachukua gunia hili la maharagwe na kuwapiga nalo.” Na kwa hivyo, sasa huo ni wakati nilipokuwa mdogo sana.

¹⁰⁷ Halafu basi, ninakumbuka kwamba wakati aliponinunulia jozi yangu ya kwanza ya viatu, a—alisema alikuwa akishuka, yeye na mama, kuvichukua. Nilikuwa miguu mitupu. Mnajua, wavulana wadogo huko chini milimani ambako nililelewa walikuwa tu na kile mnachokiita hikori ya kale, kitu kama aproni, ama, shati dogo walipokuwa mvulana mdogo. Nilivaa

hilo mpaka nilipokuwa na umri wa miaka sita, nadhani. Basi jozi yangu ya kwanza ya viatu, ilikuwa na kifuniko juu yake, ambacho kina mashimo madogo ndani yake.

¹⁰⁸ Nami sikuzote, nilipochomwa na mwiba mkononi mwangu, ningemkimbilia Mama, naye angeutoa namna *hiyo*. Nami nilifikiri hayo mashimo madogo kwenye viatu vyangu ndipo ambapo wangechukua sindano na kuitoa mahali fulani, maana Mama alisema ilimbidi ashuke “akanichukulie” jozi ya viatu. Nilifikiri alifanya hivyo kwa sindano. Kwa hiyo . . .

¹⁰⁹ Lakini baada ya vita vya dunia, nakumbuka ujumbe ulitolewa: “Kamwe hatutakuwa na vita tena. Vita vimekwisha.” Hizo zilikuwa nia nzuri; walilimaanisha hilo. Halafu basi, waliunda kile tunachojua kama Shirikisho la Mataifa, wakichukua wanaume wengi, askari, kutoka kwa kila taifa, nao wangeilinda dunia nzima. Hizo zilikuwa nia nzuri, lakini hazikufanya kazi, kwa sababu haikuwa mpango wa Mungu. Sasa, tuna kile kinachoitwa U.N. na kile ulicho: kuketi kwenye U.N. huku karibu bunduki zinakabiliana. Kamwe hautafanya kazi.

¹¹⁰ Lakini kuna kitu ambacho, wakati mmoja unaweza kukutana na wengine *wakati fulani* na kila kitu kitabadilika. Hapo ni wakati unapokutana na Mungu, na “tangu wakati huo” wewe ni mtu aliyebadilika. Mtu anaweza kukutana na Mungu na kusema, “Tangu wakati huo . . .” Hutawahi kuwa vile vile ukiisha kukutana na Yesu Kristo. Hebu nikuhakikishie kwamba: kamwe, kamwe hutakuwa vile vile ukiisha kukutana na Yesu. Ndipo sikuzote unaweza kurejea, “Tangu wakati huo . . .”

¹¹¹ Hebu tuwahoji, usiku wa leo, baadhi ya watu ambao walikutana na Mungu. Hebu tuwazie juu ya baba Ibrahimu. Alikuwa mtu wa kawaida tu. Alishuka pamoja na baba yake kutoka Babeli, wakakaa katika bonde la Shinari, katika mji wa—wa Ur, nchi ya Wakaldayo. Hakuwa kitu maalum; hakuwa mtu yeyote mtakatifu. Alikuwa mtu wa kawaida tu kama mimi na wewe.

¹¹² Ndipo siku moja, labda alikuwa mkulima, huko mashambani akilima, naye . . . au kitu fulani, ndipo siku moja, akakutana na Mungu. Hakuwa na imani zaidi kuliko mtu mwingine yeyote, lakini alipokutana na Mungu, akiwa na umri wa miaka sabini na mitano, ilibadilisha utu wake wote; kwa sababu alikutana na Mungu. Mungu akamwambia, akiwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye alikuwa amemwoa dada yake wa kambo, Sarai; na, wakati huo, alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano. Ndipo Mungu akamwambia Ibrahimu kwamba atapata mtoto kwa Sarai.

¹¹³ Sasa, hiyo ingekuwa hivyo . . . Kama ingalikuwa ni mtu fulani angalimwendea na kumwambia, baadhi ya wenzake, na

kusema, “Abramu, utapata mtoto kwa Sarai, naye atakuzalia mtoto.”

¹¹⁴ Ibrahimu angecheka, na kushikilia mbavu zake, na kusema, “Mimi, mzee kama mimi, naye mke wangu karibu miaka thelathini, au, miaka ishirini baada ya kukoma hedhi? Na nimeishi naye tangu alipokuwa na umri wa miaka kumi na saba; yeye ni tasa, na mimi mgumba. Basi tungewezaje kupata mtoto, nami miaka sabini na mitano naye sitini na mitano?” Angelicheka mbele ya rafiki yake.

Lakini alikutana na Mungu. Na tangu wakati huo, aliita kitu chochote kinyume chake kana kwamba hakikuwa hivyo. Amina. Alikuwa amekutana na Mungu.

¹¹⁵ Kama mgonjwa kamwe anaweza kukutana na Mungu, haijalishi unabaki kiwete jinsi gani, unabaki mgonjwa jinsi gani, jinsi unavyobaki kipofu, ukikutana na Mungu, kuna kitu kinachozama ndani yako, wala huoni tena hali hizi za mambo. Unaangalia aliyosema Mungu. Mungu angeweza kusema... kupata njia ya kupitia kwa masumbufu ya maisha aingie moyoni mwako, na kuweka imani humo, hakuna chochote ulimwenguni kitakachokutikisa kutoka kwake. Mtu anapokutana na Mungu, tangu wakati huo na kuendelea, yeye ni mtu aliyebadilika.

¹¹⁶ Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja, na alikuwa bado akiita kitu chochote kinyume chake kana kwamba hakikuwako. Ushuhuda ulizidi kuwa mkubwa zaidi na zaidi, ukirundikana dhidi yake; Sara alikuwa na miaka tisini naye alikuwa na mia moja. Bado alikuwa akimtukuza Mungu, mwenye nguvu, sio kusitasita kwa kutokuamini, lakini alikuwa akimsifu Mungu kila siku kwamba angempata mtoto. Kwa nini? Mungu alikuwa amekutana naye; Mungu alikuwa na rehema. Mungu alimthibitishia lile agano.

¹¹⁷ Je, tunaweza kuwa na wakati wa kuchukua thibitisho hilo, mlango wa 16 wa Mwanzo? Au tunaweza kuchukua pia, mlango wa 17? hapo alipokutana naye kwa Jina la Mungu Mwenyezi, maana yake *El Shadai*, likimaanisha ne—neni la Kiebrania, “titi la mwanamke,” *El Shadai*: “Mwenye nguvu, M—Mshibishaji, Mstawishaji,” wakati mzee, mwenye umri wa miaka mia moja, na Mungu alikutana naye, akasema, “Mimi ni El Shadai.”

¹¹⁸ Sasa, *shad* linamaanisha “titi la mwanamke” lakini *shadai* linamaanisha “mwenye matiti,” wingi. Sasa, Yeye sio Mungu mwenye “titi” tu, bali Yeye ni Mungu “mwenye matiti”: “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Ikiwa unahitaji wokovu, shikilia na unyonye kutoka kwenye titi hilo la Mungu, Neno Lake, ahadi Yake. Utakuja kujitoa kwenye njia za dhambi na utovu wa maadili, uwe mtu mtauwa, mtakatifu. Ikiwa wewe ni mgonjwa, “kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Shika tu ahadi ile nyingine ya Mungu na unyonye.

¹¹⁹ Inampasa mtoto kufanya nini? Mtoto mchanga... Sisi ni watoto wachanga wa Mungu. Nataka mpate hili, dada, ninyi nyote hapo. Sisi ni watoto wachanga wa Mungu. Basi mtoto mchanga hufanya nini wakati akiwa mgonjwa na anahangaika? Anahangaika sana na ni mgonjwa. Sasa, jambo pekee ambalo linampasa kufanya, kitu pekee ambacho kitamtuliza, ni mama amchukue, amshike kifuani mwake, na kumnyonyesha. Sasa, mama anafanya nini? Mama hutoa maziwa, naye mtoto (mtoto anayenyonya) ananyonya nguvu kutoka kwa mama hadi kwa mtoto. Kisha mtoto huimarishwa na nguvu za mama. Na tunaposhika ahadi ya Mungu moyoni mwetu, tunazinyonya nguvu za Mungu, Yule mwenye nguvu. Tunanyonya, sikuzote.

¹²⁰ Basi wazia juu ya mtoto mchanga amelazwa juu ya mama yake... kifuani mwa mama yake, ataninii... yeye huacha mahangaiko yake. Mara tu anaposhika titi la mama yake, huacha kusumbuka. Hasumbuki tena; ameridhika. Huacha kuhangaika kwake. Basi tunapoishika ahadi ya Mungu, wakati Mungu anapotufunulia: "Mimi ni Bwana aponyaye magonjwa yako yote. Yeyote atakaye, na aje." Nimelinda tumaini Lake, basi nimeridhika, kwani ninanyonya nguvu zangu tena kutoka kwa Yehova, Mwenyezi Mungu, Mpaji wa nguvu.

¹²¹ Ni kutiwa moyo jinsi gani kwa mzee, mwenye umri wa miaka mia moja, kama aliyekufa, na tumbo la uzazi la Sara, tayari limefungwa hapo alipozaliwa tasa. Na ni u—ujumbe wa jinsi gani: "Mimi ndimi Mpaji wako wa nguvu; Mimi ni El Shadai. Una umri wa miaka mia moja, lakini wewe ni mtoto tu Kwangu. Lala hapa mikononi Mwangu, na ushike ahadi Yangu; wala kamwe usione kitu kingine ila hiyo ahadi. Basi unaweza kufanya nini? Huku masharubu yakizeeka, wakati nywele zikiingia mvi, bado unaweza kunyonya na kuridhika kwamba nitatimiza Neno Langu."

¹²² Daktari anaweza kusema, "Unazidi kuwa vibaya zaidi na zaidi." Hiyo haikusumbui hata kidogo. Bado unanyonya kutoka kwenye ti—titi la El Shadai. "Mungu, ulinena moyoni mwangu; ulinipa ahadi. Pepo wote kutoka kuzimu hawawezi kuliondoa kwangu. Nimeridhika nitakuwa mzima. Ninanyonya kutoka kwa El Shadai." Amina.

Ninakuambia, ndugu, hiyo huondoa mfupa wa shingo ya kuku na kuweka uti wa mgongo mle, hakika hufanya hivyo, unapomshika Mungu.

¹²³ Wakati Ibrahimu, wakati alipokuwa akithibitisha kile kiapo, mnaona Yeye alisema, "Chukua mbu—...ko—...kondoo, kondoo dume; nipe kondoo dume, na pia nipe ndama wa miaka mitatu. Kisha chukua hizi... " Akawapasua vipande viwili, akawaweka upande mmoja. Akasema, "Nichukulie hua na njiwa mchanga."

Lakini hivi mliona...? Laiti tungalikuwa na wakati wa kuliendea. Ninaangalia ile saa. Nami, sitaki kutoka kwenye

somo langu, lakini Ibrahimu akachukua . . .

Alisema, “Wachukue hao wawili, au, hua na njiwa.”

¹²⁴ Sasa, hua sikuzote alikuwa, aliwakilisha, au, alikuwa upatanisho kwa ajili ya ugonjwa. Unaona, njiwa hawakupasuliwa; wengine walipasuliwa, kwa sababu lile—lile agano pamoja na Injili lilibadilishwa kutoka sheria likawa neema, lakini uponyaji wa Kiungu daima umebaki vile vile. Kwa uponyaji wa ukoma, walimchukua njiwa, au, hua, na kukata kichwa chake, na kuimwaga hiyo damu juu ya huyo mwingine, naye akaenda kwa ajili ya utakaso wa ukoma, akinyunyiza, akilia, “Mtakatifu.”

¹²⁵ Sasa, angalieni katika hili, njiwa hawakupasuliwa. Sasa, angalieni ishara hii. Loo, jamani. Natumaini mtalipata hili. Juu . . . Ilipofikia . . . Ibrahimu aliwafukuza ndege wote wasiikaribie, ndege wa angani, mpaka ikaninii . . . jua lilipoanza kuchwa. Ndipo wakati jua lilipokuchwa, maana yake wakati hautakuwapo tena. Kisha usingizi mzito ukamshika Ibrahimu, kama afanyavyo kila mwanadamu aliyezaliwa duniani: Tunaingia katika usingizi wa mauti. Hufi; unaenda tu, unabadilisha tu makazi yako.

¹²⁶ Sasa, usingizi mzito ukamshika Ibrahimu, naye akatazama, na mbele yake ikaenda ta—tanuru ya moshi. Kila mwenye dhambi anayekufa, na kila mtu anayezaliwa katika ulimwengu huu, huja kupitia kuzaliwa kwa kujuana kimwili, hana budi kufa. Sisi sote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, na kila mtu huzaliwa katika ulimwengu huu, mwenye dhambi. Sijali jinsi wazazi wako walivyokuwa watakatifu, unakuja katika ulimwengu huu jinsi mwenye dhambi au mtu mwingine yeyote anavyokuja. Sisi ni . . . Wewe ni mwenye dhambi. “Tumezaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo,” linasema Neno. Wewe—wewe—wewe umeshindwa kabisa kwa kuanzia.

¹²⁷ Halafu, kila mwanadamu anayekufa, kuzimu ni mahali pake pa kupumzika. Hiyo ndiyo raha yote anayopata; aliyekuja kabla ya Ibrahimu. Angalieni, ndipo zaidi ya hayo, baada ya kifo huja kuzimu, lakini zaidi ya kuzimu inakuja Nuru ndogo nyeupe. Loo, jamani. Jina la Bwana libarikiwe. Hiyo Nuru ndogo nyeupe iliyopita huku na huku kati ya dhabihu hizo.

Yeye akasema, “Unaona, Ibrahimu, nitakalofanya?” Alikuwa akilithibitisha agano pamoja na Ibrahimu. Sasa, labda nitaelezea hilo haraka.

¹²⁸ Sasa leo hii, sisi Wamarekani, tunafanyaje tunapothibitisha agano? Tunaenda kufanya mapatano ya biashara, jambo la kwanza mwajua, nitanyosha mkono na kuushika mkono wa huyo jamaa, niseme, “Nipe mkono.” Hivyo ndivyo tunavyofanya agano: “Pena. Pena mikono. Tulilithibitisha; hiyo ni kweli; tutakubaliana juu ya hilo.” Hilo ni agano.

¹²⁹ Sasa, huko Japani, mnajua jinsi wanavyofanya agano huko? Wanalizungumzia kikamilifu, halafu wanachukua kisahani kidogo kilichojaa chumvi, kisha wanarushiana chumvi. Hilo ni agano huko Japani.

¹³⁰ Lakini katika siku za Ibrahimu huko Mashariki, jinsi walivyofanya agano ilikuwa kuchukua mnyama, kama kondoo ama yeyote yule, na kumwua na kumpasua vipande viwili; na kila mmoja akapitia katikati ya vipande hivyo viwili vya yule mnyama. Sasa, mnaona kile ile Nuru ndogo nyeupe ilikuwa ikifanya? Nao wakaandika agano hili: “Ninakubali kufanya *hivi na vile*, na *hivi na vile*.”

¹³¹ Sasa, wakati walipolishika agano hili kati yao, walisema, “Kama tukivunja agano hili—kama tukivunja agano hili, miili yetu na iwe kama mnyama huyu aliyekufa ambaye tumelichukua juu yake.” Ndipo wakachukua lile agano, na kulipasua *hivyo*; mmoja, anachukua kipande kimoja, na mwingine, kingine. Havingeweza kamwe kunakiliwa.

¹³² Kamwe huwezi kunakili kipande hicho cha karatasi, hata ufanye nini. Vinapaswa kurudiana tena na kuumana, hivyo vipande vya karatasi ambavyo vimepasuliwa vipande viwili. Kamwe usingeweza kuvinakili. Mmoja, anaenda na kimoja, na mmoja, hicho kingine. Ndipo agano hili litakapothibitishwa na kuletwa, kiapo kimethibitishwa, kisha wanaleta vipande hivi viwili pamoja, na vinafanana kipande kwa kipande.

¹³³ Sasa, ni agano lipi la Mashariki Mungu alikuwa akimpa Ibrahimu? Kwamba kupitia uzao wa Ibrahimu angekuja Bwana Yesu, Yeye aliyebarikiwa. Mungu alimpeleka hadi Kalvari na kumpasua vipande viwili, akaitenganisha Nafsi Yake na mwili Wake. Nao mwili Wake, Mungu akaufufua siku ya tatu, na akautwaa na kuuweka kwenye mkono Wake wa kuume. Na kwenye siku ya Pentekoste, aliishusha Roho iliyokuwa ndani ya Yesu Kristo, lile Agano pamoja na Kanisa.

¹³⁴ Ndipo Kanisa litakapokusanyika pamoja katika ufufuo, Roho yule yule, aliyekuwa katika Yesu Kristo, aliyepasuliwa kutoka Kwake, itambidi kuwa ndani ya Kanisa. Huwezi kunakili kitu kama Huyu; huwezi kufanya kitu chochote tofauti na Huyu. Haina budi kuwa ni Roho Mtakatifu yeye yule aliyekaa ndani ya Kristo. Ndipo unyakuo utakapokuja, ule Mwili utakapokuja, Bibi-arusi Wake aliyepasuliwa kutoka Kwake, au, Roho Mtakatifu atamleta huyo Bibi-arusi apate kutoshea kabisa katika Mwili wa Yesu Kristo.

¹³⁵ Basi unaweza kuona kutoka siku za Luther, hadi Wesley, hadi Pentekoste, na sasa wakati wa mwisho, jinsi Roho huyo anavyoambika? Ishara zile zile na maaajabu yale yale aliyoyafanya hapa duniani yanafanywa Kanisani siku hizi. Ni agano hilo ambalo Mungu alifanya na Ibrahimu, nasi ni watoto wa Ibrahimu. “Tukiwa wafu katika Kristo, tunachukua uzao wa

Ibrahimu na ni warithi sawasawa na ahadi.” Tangu wakati huo, Kanisa lilikuwa na agano. Naam, lilikuwa ni tofauti.

¹³⁶ Sasa, wakati Musa, nabii mtoro nyuma upande wa nyuma ya jangwa... Mtu huyo alizaliwa kuwa nabii. Naye alikuwa mtu mashuhuri; alisomea mafanikio ya jeshi. Lakini alijaribu kutekeleza hayo kwa akili zake zote. Mbona, alikuwa mtu mwerevu sana, angeweza kuwafundisha hao walimu wa Misri. Alikuwa mtu mwerevu. Sasa, huko nyuma upande wa nyuma ya jangwa, vipi kama alisema, “Nilishindwa, kwa hivyo watu wangu bado wako utumwani. Labda afadhali nisome kidogo hisabati yangu, au juu ya mbinu yangu ya mbinu ya kijeshi, ama chochote kile. Nitashuka, nichukue miaka miwili zaidi ya shule, na labda nitaweza kuwakomboa watu wangu.”

¹³⁷ Hiyo ni akili tu ya yeye kufanya hivyo kadiri ingalikuwa kumpeleka mtu kwenda kujifunza kuwa mhubiri. Mungu huwaita watu hata kama hawezi kutofautisha maharagwe na kahawa iliyopasuliwa. Inaleta tofauti gani? Maadamu anamjua Kristo, hilo ndilo jambo muhimu, kama alipata kukutana Naye.

¹³⁸ Afadhali niwe na mtu akiwa na mmoja wa watoto wangu huko nje katika e—eneo la vichaka, mahali fulani huko chini karibu na kisiki cha kale, ambaye hata hakujua ABC zake au kujua ni upi mkono wake wa kulia wala wa kushoto, ikiwa anamjua Yesu Kristo, ningependa awe karibu na mtoto wangu, kabla sijawa na profesa yeyote anayejua theolojia chungu nzima, wala hajui zaidi juu ya Mungu kuliko vile sungura anavyojua juu ya viatu vya theluji. Ningetaka...

¹³⁹ Nakuambia, ndugu, tunachohitaji leo ni kurudi kwenye Biblia na ubatizo wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu kurudi kanisani, na mengi ya upuuzi huu mwingine yamekatiliwa mbali.

¹⁴⁰ Sijaribu kuunga mkono ujinga. Namaanisha, endapo umepata elimu pamoja na hiyo, amina. Lakini agano la elimu litaanguka moja ya siku hizi, lakini agano pamoja na Mungu litadumu milele, na milele, na milele. Litaendelea kupitia dahari za wakati hadi Umilele.

¹⁴¹ Sasa, Musa, hakupaswa kung’arisha chochote; kitu pekee kilichompasa kufanya ni kukutana na Mungu. Basi siku moja, Mungu alishuka akachukua kichaka kimoja huko nje, akasema, “Njoo huku, Musa. Nataka kuongea nawe.” Mnajua, ni jambo fulani la kigeni kuhusu, Musa angeweza kusema, “Tangu wakati huo, kitu fulani kilitukia.”

¹⁴² Mwangalieni. Alikuwa ametulia huko chini nyuma ya mlima, chini kabisa ya mlima. Na alipofanya hivyo, alioa mwanamke mrembo wa Kushi, naye alikuwa na sura nzuri; pia alikuwa na mtoto mdogo wa kiume, aliyeitwa Gershomu. Na loo, alikuwa anaendelea tu vizuri. Alikuwa ameo kuhani—kuhani wa Midiani, binti ya Yethro, Zipora, nao walikuwa wanaendelea

vizuri, alikuwa na familia ndogo nzuri, alikuwa na kondoo wengi. Naye alikuwa akiendelea sawa tu, kwa hivyo aliwaacha hao watu waendeleo.

Lakini Mungu alipokutana naye, alimbakilisha. Mwangalie pale, huyu mchungaji mkuu wa kondoo kule nyuma, lakini asubuhi...

¹⁴³ Unajua, vitu vingine... Jambo moja kulihusu, wakati mtu anapokutana na Mungu, daima unaweza kujua. Atafanya mambo ya kipumbavu zaidi kwa yale aliyokuwa akifanya. Mwangalieni Musa. Sasa, Musa, kesho yake asubuhi baada ya kukutana na Mungu katika kichaka hiki kilichowaka moto na Mungu akamwambia ashuke kwenda Misri...

Yeye alisema, "Kwanza, nionyeshe utukufu Wako." Ndipo akamwonyesha uponyaji wa Kiungu, jinsi alivyoweza kuuponya mkono wake wenye ukoma.

¹⁴⁴ Naye alikuwa anashuka kwenda Misri. Sasa angalieni, kesho yake asubuhi, huyu hapa akishuka kwenda zake. Sasa, alikuwa na umri wa miaka themanini. Unajua, ilimchukua miaka arobaini kushindilia theolojia ndani yake kwa elimu; ikamchukua Mungu miaka arobaini kuiondoa kwake. Hiyo ni kweli, kumtoa kile ulimwengu ulikuwa umeweka ndani yake. Lakini Mungu anaweza kukufanyia kwa sekunde arobaini, ikiwa tu utamruhusu afanye hivyo. Lakini basi...

¹⁴⁵ Sasa, huyu hapa kesho yake asubuhi. Siku moja mwanachuoni hodari, hekima yote ya Wamisri, na kesho yake asubuhi, mwangalie mwanachuoni huyu. Ana mkewe aliyeketi kumtagaa nyumbu; ana mtoto mchanga nyongani mwake. Na hapa yuna ndevu kubwa, ndefu, jozi ya ndevu namna *hii*, kichwa chake chenye upara kiking'aa, fimbo mkononi mwake, akishuka, huku anachechemaa, "Utukufu, utukufu."

"Unaenda wapi, Musa?"

"Ulisema nini? Haa?"

"Waenda wapi?"

¹⁴⁶ "Nashuka kwenda Misri kuiteka": uvamizi wa mtu mmoja. Lakini alifanya hivyo. Alifanya hivyo. Kwa nini? Alikutana na Mungu. Na shida zilipokuwa ngumu, na—na... kila kitu kilikuwa kinaenda mrama, alikumbuka alikuwa amekutana na Mungu katika kile kichaka kilichowaka moto. Hiyo iliwaka moto moyoni mwake, haidhuru Wamisri walikuwa wabaya kiasi gani, na kiasi gani wasingewaruhusu hao wana waende, ni mara ngapi waliguna jangwani, na kusema, "Laiti Mungu..." na wakataka kumpiga mawe, na, "Tunataka vyungu vya nyama vya Misri." Hilo halikumsumbua hata kidogo. Alisonga mbele kuelekea nchi ya ahadi, kwani alikuwa amekutana na Mungu katika kichaka kilichowaka moto. Naam, bwana.

¹⁴⁷ Alikuwa ni maskini bikira Mariamu, msichana mdogo tu wa kawaida, katika mji mbaya kuliko huu. Lakini hata hivyo hakuvuta sigara wala kunywa pombe; alikuwa bikira. Ndipo yeye, siku moja, alikuwa njiani na, pengine, ndoo ndogo chini ya mkono wake, akishuka kwenye kisima cha umma ku—kuchota maji, ugavi wa maji wa kila siku.

¹⁴⁸ Hebu tumwazie tu akienda kando ya barabara, akitembea, akiongea, au, akijiambia mwenyewe, labda wimbo mzuri: “Bwana ndiye Mchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza; Yeye hunihuisha nafsi yangu.”

¹⁴⁹ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... ilikuwa ni gudulia katika siku hizo, badala ya ndoo. Ndipo mara moja Nguzo kubwa ya Moto ikashuka mbele yake. Kutoka kwenye moto huo akaja Gabrieli, Malaika Mkuu, akasema, “Salamu, Mariamu.” (Hiyo inamaanisha, “simama; ngoja kidogo.”) “Simama, Mariamu. Umepata kibi kati ya wanawake. Umepata kibali kwa Mungu, nawe utapata Mtoto, bila kumjua mwanamume.”

Kasema, “Litakuwaje neno hili?”

Akasema, “Roho Mtakatifu atakutia uvuli. Nacho hicho Kitu kitakachozaliwa kwako kitaitwa Mwana wa Mungu.” Amina.

¹⁵⁰ Tangu wakati huo na kuendelea, Mariamu alikuwa mwanamke tofauti. Maskini bikira huyo mwoga akienda kila mahali akishuhudia, “Nitapata Mtoto, bila kumjua mwanamume.”

¹⁵¹ Yeye hakusubiri hadi awe na hakika; hakungojea mpaka ahisi uhai; hakusubiri hakikisho lolote. Neno la Malaika lilimtoha. Alikuwa amekutana na Mungu. Sasa, vile... Kama mngeweza kufanya hivyo sasa, kama tungekuwa na akina Mariamu wengi zaidi hapa usiku wa leo, kama tungalikuwa na akina Mariamu ambao hawakusema, “Ngoja nione kama nimepata nafuu kidogo, kabla sijasema chochote.” Kabla ya kuhisi chochote, au chochote kingine, aliamini tu Neno la Mungu na kuanza kumsifu kwa ajili yake. Loo, jamani. Hebu tumfuatilie dakika chache. Hebu tumwone upesi sana.

Alikuwa na bi—binamu jina lake Elisabeti. Naye Elisabeti... Malaika alimwambia, akasema, “Binamu yako, maskini nanii wa Elisabeti...”

¹⁵² Zakaria alikuwa kuhani, akakutana naye hekaluni, amesimama mkono wa kuume wa madhabahu, na kumwambia kuwa atapata mtoto kwa Elisabeti. Na atachukua mimba baada ya siku za huduma zake huko hekaluni. Naye...

¹⁵³ Mbona, alishuku. Hilo... wazieni tu basi, kuhani huyo mzee alikuwa na mifano mingi sana: kama vile Hana hekaluni; na—na Sara, ndiyo kwanza tuzungumze habari zake; wakongwe na

kujifungua watoto. Kasema, “Lo, hii haiwezekani. Mke wangu ni mkongwe sana.”

Alisema, “Mimi ni Gabrieli anayetoka kwa Mungu. Utakuwa bubu mpaka siku mtoto atakapozaliwa. Utamwita jina lake ‘Yohana.’”

¹⁵⁴ Naye alikuwa bubu. Naye akaenda huko kwa mkewe. Akapata mimba, naye. . . ilimchukua miezi sita pasipo na uhai wowote katika huyo mtoto, naye alikuwa na wasiwasi sana.

Kwa hiyo Mariamu alikuwa amesikia juu ya jambo hili. Kwa hiyo naona maskini mashavu yake mekundu vivyo hivyo; alikuwa akienda zake, mwenye furaha tu kadiri alivyoweza kuwa; hakuna hisia bado.

Yesu kamwe hakusema, “Je, ulihisi?” Alisema, “Je, uliamini?” Unataka kuamini, wakati unapoamini.

¹⁵⁵ “Jinsi neema hiyo ilionekana kuwa ya thamani, ile saa niliyohisi kwanza”: hilo halisikiki kuwa sawa, sivyo? “Saa niliyoamini kwanza; nilipomwamini Mungu.” Hivyo ndivyo ule uthamani, iliyoufanya. Loo, Mungu akionekana usiku baada ya usiku katika mikutano na kuonyesha ishara kubwa na maajabu; loo, inapaswa kuichochea tu mioyo yetu. Hakika. “Jinsi imani hiyo ilivyoonekana ya thamani, neema, ile saa niliyoamini.”

¹⁵⁶ Huyu hapa Mariamu akienda, mashavu yake madogo mekundu vivyo hivyo, macho yake madogo yakimetameta, maangavu, alijiandaa, na huyo akakwea vilima vya Yuda, huko juu mahali bi—binamu yake alikoishi. Nami naweza kumwona Sara. . .

¹⁵⁷ Ninawaona wanawake huko nje mtaani. . . Nikila chakula cha jioni leo hii, ninge—ninge. . . Wangalinitupa nje ya mkahawa kama sikuwa nimegeuza mgongo wangu. Mwanamke alikuja pale (angejifungua wakati wowote) akiwa amevalia maskini kaptura hizi, maskini kizee kikubwa, loo, huku akivuta sigara; naye daktari anasema ni mojawapo ya vitu vya kufisha sana. Sikiza, ndugu, hiyo ni hujuma. Hakika ndivyo ilivyo. Na onyo la madaktari kwamba kansa ya koo na mapafu; na kuvuta hiyo moja kwa moja hadi kwenye yule mtoto mle ndani. Lakini huko. . .

¹⁵⁸ Lakini wanawake walikuwa tofauti katika siku hizo. Aliingia na kujificha, asionekane na wanaume, ndipo akaingia ndani akajificha. Na alikuwa mle ndani kwa—kwa miezi sita; mtoto Yohana hakuwa amejongea; aliumbwa katika tumbo la mama yake; tunajua hiyo kwa jumla si kawaida.

¹⁵⁹ Kwa hivyo anaweza kuwa aliinua dirisha na kutazama nje *hivi*, pazia, ndipo akamwona mwanamke mrembo akija, yapata umri wa miaka kumi na minane. Akaangalia tena.

"Loo," akasema, "huyo ni Mariamu; loo, jamani." Naye akachukua shali yake ndogo akajizungushia, akakimbilia huko mbio sana.

¹⁶⁰ Naye mumewe alikuwa bubu wakati huo; hakuweza kuongea. Akatoka mbio na kuchukua hii... akachukua hiyo shali ndogo na kujizungushia, akatoka mbio. Alikuwa ameketi kule nyuma, akishona vijibuti vidogo na kadhalika, mwajua, akijiandaa, mwajua, blanketi ndogo, ushonaji. Na kwa hiyo akatoka mbio, na kusema, "Loo, Mariamu."

Katika siku hizo, mnajua, walikumbatiana; walipendana. Siku hizi, huupati tena. Unaona?

¹⁶¹ Nilikuwa katikati ya mji. (Mke wangu hayupo hapa usiku wa leo. Nimelisimulia wakati yeye akiwa hapa.) Kweli, nilikwenda katikati ya mji, hapa si muda mrefu uliopita, ndipo dada fulani akasema, "Aloo, Dada Branham."

Nikasema, "Hukumzungumzia."

Akasema, "Naam, nilimzungumzia."

"Vema," nikasema, "alikusikiaje huko mtaani, nami nimeketi papa hapa karibu nawe wala sikusikia?"

"Loo," akasema, "Nilitabasamu."

Nikasema, "Maskini tabasamu la kipumbavu, hilo si kitu. Jamani, kwa nini hukuongea na huyo dada?"

¹⁶² Nachukia kuona upuuzi huo. Wakati fulani uliopita, nilikuwa huko chini Florida, na kulikuwa na—na... Tulikuwa tukifanya mkutano huko nje kwenye namna fulani ya uwanja unaomilikiwa na mwanamke wa kifalme. Nao wakasema... mmoja wa mameneja akaja na kusema, "Huyo mwanamke wa kifalme anataka kukuona."

"Vema," nikasema, "yeye ni nani?"

Akasema, "Mbona, yeye—yeye ni mwanamke mashuhuri hapa. Ni mwanamke wa kifalme."

Nikasema, "Vema, yeye ni mwanamke tu, sivyo?"

Kasema, "Naam."

¹⁶³ Vema, nikasema, "Vema sasa, kama mtanipa wakati wa kuzungumza naye, vipi kuhusu baadhi ya maskini watu hawa wagonjwa huku nje wanaonitaka zaidi?" Mnaona? Kisha nikasema, "Je, vipi kuhusu wakati wao?" Unaona?

"Loo," kasema, "lakini yeye—yeye ataninii... Nitamleta tu nyuma ya jukwaa."

¹⁶⁴ Nami nikaondoka. Alikuwa amesimama pale na jozi ya miwani mkononi mwake kwenye kijiti, ameishika namna *hiyo*. Sasa, mtu yeyote mwenye akili anajua usingeweza kuona kwa—kwa miwani unayoishikilia namna *hiyo*, mnaona. Mwanamke mkubwa mno amejipamba vito vya kutosha kwenye kifundo

cha mkono wake kumtuma mmishenari kote ulimwenguni mara tano. Naam, bwana. Yamening'inia . . .

Naye akasema, “Je, wewe ni Daktari Branham?”

Nikasema, “Hapana, mama; hapana.” Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

“Loo,” akasema, “Nimevutiwa.” Naye akanyanyua mkono huo mkubwa juu *hivi*.

¹⁶⁵ Sasa, ningependa hilo, nilinyosha mkono na kuushika huo mkono mkubwa mnene na kuushusha chini. Nikasema, “Nina furaha kukufahamu.” Nikasema, “Ushushe chini hapa nipate kukufahamu wakati mwingine nitakapokuona.” Mnaona?

¹⁶⁶ Hiyo ni kweli. Ninapenda kupeana mkono kuzuri kwa mtindo wa kale wa mkono mchangamfu. Na—na—napenda watu wawe tu jinsi walivyo. Acheni kuiga kwa wingi hawa “Mbwa wa Kimarekani” kama tunavyowaita. Sisi ni Wakristo. Hebu tuishi kama Wakristo na tuwe askari wanaume na wanawake, wa msalaba. Upuuzi huu wote hapa; tabasamu dogo. Huh, napenda huko kupeana mikono kuzuri, ambako unakuhisi.

¹⁶⁷ Paul Rader alisema wakati mmoja, alikuwa amemwacha mke wake ameketi tu mezani, nao walikuwa na ugomvi kidogo juu ya mahali fulani alipotaka kumpeleka. Paul Rader mashuhuri, mwajua, naye ni rafiki msiri wangu, basi alikuwa amesema kidogo a—alishikwa na hasira, hivyo basi a—akaenda mlangoni, naye mkewe sikuzote angengojea pale na kumbusu kwaheri. Ndipo angeshuka kwenye vipandio, na kwenda nje hadi mwisho wa . . . na kumpungia mkono namna hiyo, kisha anaenda zake kazini.

¹⁶⁸ Akasema walikuwa na ugomvi kidogo mezani kuhusu jambo fulani. Naye akasimama mlangoni, kasema alisema “*busu* Kwaheri.”

Mke akasema, “Kwaheri.”

Akatoka akaenda huko nje kisha akageuka langoni, akampungia mkono, akasema mke alikuwa amesimama mlangoni, analia. Akasema, “Kwaheri.”

Naye mke akasema, “Kwaheri.”

¹⁶⁹ Akashuka mtaani na kusema alianza kufanya kazi moyoni mwake, Roho Mtakatifu alimshika, mwajua, akaanza kufanya kazi moyoni mwake. Naye akasema, “Loo, vipi kama angekufa wakati nimeondoka? Vipi kama angeanguka afe? Vipi kama mimi ningekufa? Vipi kama ningegongwa mtaani huku Fort Wayne kabla kamwe sijapata kurudi? Ningefanya nini?” Namna hiyo, akilizungumzia namna hiyo. Loo, jamani. Kasema, yeye alisema, “Loo, nilihukumika sana; sikujua la kufanya.” Akasema, “Nikarudi nyuma haraka sana, nikalifungua lango upesi, na kukimbilia ndani, na kuufungua mlango kwa nguvu,

akasema . . . nikaangalia kote na kusema, 'Helen, uko wapi? Uko wapi?'"

¹⁷⁰ Kasema, "Nilisikia '*nusa, nusa*,'" Kasema, "Alikuwa amesimama nyuma ya mlango." Kasema, "Nikamtazama namna hiyo." Kasema, "Kamwe sikusema neno." Kasema, "Nilinyosha tu na kushika mikono yangu, na kumbusu. Ndipo nikasema, '*busu Kwaheri*.' Mke akasema, 'Kwaheri.'"

¹⁷¹ Kwa hivyo alikimbia nje ya lango kisha akageuka, akatazama nyuma. Akasema, "Alikuwa amesimama ndani, mlangoni, nami nikasema, 'Kwaheri,' naye akasema, 'Kwaheri.'" Kasema, "Alipunga mkono kama vile alivyofanya mara ya kwanza, lakini mara ya pili alikuwa na hisia ndani yake." Basi hivyo tu ndivyo . . .

¹⁷² Hivyo ni karibu vile kumtumikia Bwana, mnajua. Huna budi kuweka moyo wako ndani yake; huna budi kuwa mwaminifu. Huna budi kukutana na Mungu, sio kwenda kanisani na kufanya maungamo baridi, ya macho makavu; kushuka chini pale na kukaa huko chini.

¹⁷³ Nililelewa katika kanisa la Baptisti; mnajua hilo. Wala hatukuwa Wabaptisti kama ninyi nyote Wabaptisti hapa: Unaenda kule na kupeana mikono, na kushika mkono wa kulia wa ushirika, kisha unaandika jina lako kwenye kitabu, na ubatizwe. Tulishuka madhabahuni na tukapigana-pigana mgongoni hata tukafaulu; tulipata kitu, ndugu. Namaanisha, mnahitaji zaidi . . . Mnahitaji Wabaptisti wa Kentucky, Wabaptisti wa Kimishenari wa kale huku nje. Nawaambia wao . . . Tofauti pekee niliyoona kati yao na Wapentekoste, hawakukubali kunena kwa lugha; hayo ndiyo yote niliyojua. Wao . . .

¹⁷⁴ Tulifaulu; tulikaa pale madhabahuni, nao akina mama wakongwe wametuzunguka wakilia na kuomba, wakitupigapiga mgongoni ndipo jambo fulani likatukia. Tulikaa hapo mpaka tukafa, kisha tukazaliwa mara ya pili, na tukawa kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Naam, bwana. Ni vibaya sana tuliondoka. Inatubidi kukutana na Mungu. Mtu anapokutana na Mungu, ni tofauti. Yeye ni—yeye ni mtu tofauti tangu hapo na kuendelea.

¹⁷⁵ Kulikuwako na mwenye ukoma wakati mmoja, amejaa tu ukoma. Ndipo basi alipokutana na Mungu, tangu wakati huo na kuendelea, hakuwa na ukoma. Kulikuwako na mwanamke mwenye sifa mbaya aliyekuja kisimani wakati mmoja kuchota maji, naye akamwona M—Myahudi ameketi upande ule mwingine. Ndipo akashusha gudulia; alikuwa mwenye sifa mbaya sana asingeweza kutoka pamoja na wanawake waadilifu. Waliwabagua wakati huo; hawawabagui sasa. Kwa hiyo wakaninii tu . . . Hiyo ni jamii. Kwa hiyo walishusha tu kisima . . . ndoo chini kisha wakaanza kuivuta juu namna *hiyo*.

¹⁷⁶ Basi alipofanya hivyo, alimsikia mtu Fulani akisema, “Nipe maji ninywe, mwanamke.” Ama, “Mwanamke, nipe maji ninywe.” Hivyo ndivyo alivyosema, maana kitenzi huwa kabla ya kielezi katika nchi hiyo. Lakini akasema, “Nipe maji ninywe.”

Na kwa hivyo, akasema, “Si kawaida kwenu nyinyi Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho. Hatuna desturi sisi kwa sisi.”

Akasema, “Lakini kama ungejua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Ningekupa maji usije hapa kuteka.”

“Mbona,” akasema, “kisima ni kirefu basi Wewe utawezaje. . . Utachota na nini kwa vyovyote vile?”

Akasema, “Maji nitoayo ni Uzima, Uzima wa Milele unaobubujika katika nafsi.”

“Mbona,” akasema, “baba—baba zetu waliabudu katika mlima huu, Ninyi mnasema ni huko Yerusalemu. . .”

¹⁷⁷ Naye akaendelea na—na mazungumzo mpaka akashika roho yake. Alipoishika roho yake, Yeye alisema, “Vema, nenda kamwite mume wako mje naye hapa.”

Yeye, kumbukeni, alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya. Kwa hiyo alisema, “Nenda kamwite mume wako mje naye hapa.”

“Mbona,” akasema, “Sina mume yeyote.”

Akasema, “Umesema kweli. Maana unao watano, naye unayeishi naye sasa siye mume wako. Hapo umesema kweli.”

¹⁷⁸ Mtazameni mwanamke huyo. Upesi, alikuwa amekutana na Kitu, Kile hasa mnachokutana nacho kila usiku. Kingeweza kukubadilisha kama kilivyombadilisha yeye? Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.” Ilikuwa ni tofauti ya jinsi gani kwa yule, kwa yule kuhani aliyesema Yeye alikuwa ni Beelizebuli. Alikuwa amefunzwa vizuri kuliko nusu ya wahubiri; ingawa ni kahaba.

¹⁷⁹ Kasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua, sisi Wasamaria tunatazamia Masihi kuja; Yeye atakuwa ni Nabii-Mungu. Atakuwa ni Masihi, bali Yeye atatwambia mambo haya. Atafanya kazi za namna zizi hizi hapo Yeye atakapokuja.”

Hiyo ni ishara ya Masihi? Ilikuwa wakati huo. Mnaona?

Kasema, “Tunajua. . . Ninajua ya kuwa Wewe ni Nabii; najua ndivyo ulivyo. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatuambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe?”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁸⁰ Sasa, ninataka kafiri aniambie wakati mmoja ambapo Yesu alisema. . . Makafiri wengi wanawaambia, “Yesu kamwe

hakudai kuwa Mwana wa Mungu.” Alikiri pale; naam. Alisema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

¹⁸¹ Na upesi akaiacha ile ndoo, na tangu wakati huo, tangu wakati huo, alijua ya kuwa Masihi alikuwa duniani. Loo, jamani, laiti tungalifanya jambo lile lile usiku wa leo. Laiti tungalitambua kwamba Yeye hajafa. Yu hai milele; Yeye anaishi kufanya uombezi. “Kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.” Roho Wake yuko ndani yetu; Roho Wake yuko miongoni mwetu.

¹⁸² Tangu wakati huo, watu wa huo mji wakamwamini Mungu kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke. Yesu hakufanya hivyo tena kule chini; Yeye alishuka tu chini, akalifanya mara hiyo moja, na Samaria yote ikamwamini. Hakuwahi kuwa na ibada hata moja ya uponyaji; alikuwa akihifadhi hiyo kwa Filipo. Lakini tangu wakati huo na kuendelea, mwanamke huyo alibadilishwa; mji huo ukabadilishwa.

¹⁸³ Wakati mmoja mvuvi mzee, amejizungushia aproni chakavu iliyojaa grisi, ndugu yake, Andrea, akamleta mbele za Yesu. Na mara tu alipofika mbele za Yesu, Yesu alisema, “Jina lako ni Simoni; wewe ni mwana wa Yona.” Na tangu wakati huo, tangu wakati huo, huyo alikuwa ni mtu tofauti.

¹⁸⁴ Filipo akaenda akampata Nathanaeli na kumleta Kwake, Naye akasema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Rabi, ulinijua lini?”

¹⁸⁵ Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Na tangu wakati huo, tangu wakati huo, alikuwa mtu aliyebadilika. Kila mtu hubadilishwa anayewahi kukutana na Mungu.

¹⁸⁶ Kulikuwa na Myahudi mdogo wa kale aliyekuwa na pua iliyopinda. Kanisa lenye zile funguo lilikuwa limefanya kosa kubwa sana. Walikuwa wamezunguka na kusema, “Sasa, na tuje pamoja.” (Tutaona zile funguo zilikuwa na faida gani.) Walizunguka na kusema, “Hebu sote tuje pamoja na kuchagua mtu mmoja ambaye ameingia na kutoka miongoni mwetu tangu mwanzo kuchukua nafasi ya Yuda, kwa sababu imeandikwa katika Maandiko, ‘Kikao chake kiwe ukiwa na sehemu yake ichukuliwe na mwingine.’”

¹⁸⁷ Nalo lilisema walipiga kura, nayo ikamwangukia Mathiya; kamwe hakufanya jambo lolote. Hilo lilikuwa ni chaguo la mwanadamu. Ndipo Mungu akashuka na kumchukua maskini jamaa mdogo mbaya sana aliyekuwako mjini kuchukua mahali pake, maskini Myahudi mdogo.

Alisema, “Nitamwonyesha tu kile nitakachomfanya anifanyie.”

¹⁸⁸ Naye alimwangua Stefano alipokufa, hilo kwa namna fulani lilimwangua sana. Ndipo muda si muda mwajua, alikuwa akishuka kwenda zake. Alikuwa na barua mfukoni, alisema, “Nitawashika hao watakatifu wote wanaojibingirisha. Ninayo barua papa hapa kutoka kwa kuhani mkuu. Nitashuka kwenda Dameski, na nitawatupa gerezeni; nitafanya kila niwezalo. Nitakomesha huko kupiga makelele, na mayowe, na vurugu hiyo yote, kunena kwa lugha, na kadhalika. Nitapata amri; nitafanya hivyo.” Maskini pua hiyo ikining’inia chini namna *hiyo*.

Mungu akasema, “Nitakutana naye tu barabarani na kumbadilisha.”

¹⁸⁹ Karibu adhuhuri, alikuwa akija katikati ya barabara, ndipo muda si muda mwajua, Nguzo hiyo ya Moto ikatokea mbele yake, na kusema, “Sauli, Sauli, mbona wanitesa?”

Akaanguka chini. Akasema, “Bwana, ni Nani ambaye ninamtesa? Jina Lako ni nani?”

Akasema, “Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kupiga teke michokoo.”

Basi tangu wakati huo, aliitupa barua yake na akawa mmoja wao; tangu wakati huo. Naam, ilimbadilisha.

¹⁹⁰ Anania akamwekea mikono kwa ono aliloona, naye akapata kuona, akampeleka mpaka mto Dameski na kumbatiza. Akawa ninii . . . mtakatifu kwa ajili ya kanisa la Mataifa. Mungu . . .

¹⁹¹ Sasa, angalieni hapa. Vipi . . . Vipi kama walisema, wakati Paulo alipoongoka, labda kanisa lilisema, “Loo, angalieni kile tulicho nacho sasa. Tunaye huyu Paulo mashuhuri. Tunajua ya kwamba mtu huyo aliketi chini ya Gamalieli; yeye ni mmoja wa walimu hodari sana nchini. Naye ni Mfarisayo; yeye ni . . . loo, ni mtu mashuhuri. Tutamweka huko Yerusalemu, nasi tutamfanya kuwa mkuu wa kanisa kule juu. Na tutamchukua Petro, bila shaka yule aliye na zile funguo; yeye hana elimu, hawezi . . .” Biblia ilisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa. “Naye anazo zile funguo, kwa hiyo tutamtuma tu kwa Wamataifa maskini, bubu. Hao ni—hao ndio tutakaomtuma kwao pia. Kwa sababu anafanya miujiza mingi, lakini huyu mtu mashuhuri mwenye akili; tutamleta hapa juu pamoja na umati wa wasomi.”

¹⁹² Huh, Roho Mtakatifu alimtuma Paulo kwa wale bubu, na kumfanya asahau yote aliyowahi kujua, akamchukua Petro, yule bubu, akamtuma kwa wasomi. Shida ilikuwa ni nini? Walikutana na Mungu, na tangu wakati huo usomi haukuhesabiwa, sawa. Tangu wakati huo, kumbukumbu ilibadilishwa. Jinsi Mungu hufanya mambo kinyume tu na fikira za mwanadamu. Loo, jamani. Ni . . . Yeye ni ninii sana . . . Yeye hufanya mambo kwa urahisi sana. Naam, Paulo alikuwa mtu aliyebadilika.

193 Kulikuwa na kipofu, tulihubiri juu yake hivi majuzi usiku, aliyeketi langoni, akiomba sadaka. Naye akakutana na Mungu, na tangu wakati huo na kuendelea, aliweza kuona. Kulikuwa na mwendawazimu huko Gadara, ambaye angerarua nguo zake mwilini mwake, alitaka kuishi makaburini. Hapo ni mahali pazuri kwa pepo. Kwa hivyo alilala huko nje, na wangemfunga kwa minyororo. Alikuwa na nguvu sana. Angalia mtu. . .

194 Je, umewahi kumuona mtu mwendawazimu? Mbona, yeye ni mara mbi-. . . nguvu zake mara tatu, au nne. Na ikiwa nini, ukijisalimisha hivyo kwa ibilisi angekupa nguvu mara nne ya nguvu zako, ungekuwa nini kujisalimisha kwa Roho Mtakatifu? Nguvu zako zingekuwa mara elfu ngapi. Usiogope. Kwa nini? Unatembea katika Jina la Bwana Yesu; huo ndio upako. Kutana na Mungu upate kujua kinachotendeka.

195 Huyu mwendawazimu alikimbia huko nje. Ibilisi akasema, “Nenda ukamchukue yule mtu mdogo anayeonekana mwembamba anayekuja pale, mabega yake yameinama.” Kasema, “Nenda ukamshike maskini yule jamaa mdogo kule chini. Angalia watu hao wote wakitazama mahali alipo.” Kasema, “Shuka ukamshike.”

196 Huyu hapa anakimbia nje, na alipofanya hivyo, akakutana na Mungu. Na tangu wakati huo na kuendelea, akavaa nguo zake naye alikuwa na akili timamu. Ati nini? Alipokutana na Mungu! Marafiki, kuna wakati unapokutana na Mungu, hubadilisha kila mtu.

197 Kwa muda kidogo tu, nitafanya maungamo sasa. Ninawatakeni msikilize hili. Nimekuwa mhudumu miaka thelathini na mmoja. Ninafunga baada ya ushuhuda huu. Sijawahi kuogopa kifo tangu nimekuwa Mkristo. Lakini kilichonitia hofu, au, kilichonitia wasiwasi, kilikuwa ni wakati, kama ninge kufa kabla ya Yesu kuja, sikutaka kuwa ro-roho. Si—sikuzote nimehofia chochote kinachoonekana kama mzuka; ni—ni—ninakiogopa. Kwa hivyo, ni—ni—nilidhani wakati ni—ni—nikiujuu mwili huu. . . Nilifikiri ningeenda kuwa pamoja na Bwana, lakini labda ningemwona mmoja wa ndugu zangu. Na hapo wangepita kama wingu dogo jeupe, roho, nafsi ya mtu huyo.

198 Ningesema, “Loo, pale—yule pale ndugu yangu. Loo, laiti ningaliweza tu kumpa mkono. Hana mkono wowote; umeozea huko chini kaburini. Kama ningeweza kusema, ‘Aloo,’ lakini hana. . . siwezi kupata. . . sina ulimi; ulimi wangu umeozea chini kaburini. Laiti ningaliweza kumkumbatia, lakini sina. . . Mimi—mimi ni roho.”

199 Loo, hiyo ilinishtua sana. Kamwe si—sikuipenda hiyo. Na mimi—mimi—mimi ni mtu asiyejua kusoma na kuandika, na ni—ninasoma kwa shida sana, nina elimu ya darasa la saba. Na

kwa hiyo basi nikawaza, “Vema, jamani, laiti ningaliweza tu... Natumaini nitaishi hata Bwana ajapo.”

²⁰⁰ Sasa, najua atakaporudi, mwili wangu utafufuliwa. Najua kwamba nitakuwa na mwili; uzee wote utakuwa umeondoka. Hutawahi kuwa mzee huko. La, bwana. Kila dalili ya dhambi itaondolewa, na uzee ni dalili ya dhambi. Kwa hiyo, kila kitu kilichowakilisha dhambi kitaondolewa, kwa sababu kutoka kwenye ile laana. Sio kwamba ulitenda dhambi, lakini wewe ni mmoja wa jamii ya Adamu, nawe—nawe unarudi mavumbini.

Basi nikafikiria, “Laiti ningaliishi kumwona Yesu akija.”

²⁰¹ Nilimwambia Ndugu Gene hapa, Ndugu Leo na hao wengine, mara nyingi, na Ndugu Fred, wengi wa marafiki zangu, ningesema, “Loo, natumai nitaishi kumwona Yesu akija, maana atakapokuja, nitabadilishwa, wala haitanilazimu kuwa mzuka huo. Sitaki kuwa hivyo. Hapana, bwana.” Ni—nikasema, “Ngingekuwa, nadhani ni sawa, lakini na—nataka kupeana mikono. Nawapenda wanadamu. Sijui chochote ila wanadamu, kwa hiyo ni—ningependa kuwa hivyo.”

²⁰² Basi hivi majuzi asubuhi, kama wiki tano zilizopita sasa, nilikuwa huko nje mkutanoni, nikirudi. Nilikuwa nimechoka, nami nikaamka chumbani karibu saa moja. Ndipo nikasema, “Tutashuka twende maskanini asubuhi ya leo, au asubuhi,” kwa mke wangu. Naye alikuwa bado amelala, nami kwa namna fulani nikainuka, kichwa cha kitanda, nikaweka mikono yangu nyuma *hivi*. Nami nilikuwa tu nimelala pale, nikiwazia. Nikasema, “Hei, nina umri wa miaka hamsini. Sijamfanyia Bwana chochote, bado. Sina budi kuharakisha na kufanya jambo fulani.” Kisha nikasema, “Nina... ni—nitakuwa mzee baada ya muda kidogo.” Pia nikasema, “Si—sina budi kuharakisha na kufanya kitu; sijamfanyia Bwana chochote.”

²⁰³ Nilisema, “Lakini unajua, hakika ningechukia... Ninachukia wazo la kufa kabla ya Yeye kuja.” Nilisema, “Kama angekuja tu...” Nikasema, “Na—nahofia sana wazo hilo, endapo itanilazimu kuondoka ikiwa atakawia miaka michache bado, na labda sitaishi kukuona, na nitalazimika kufa na kuwa roho.” Mmm, sikupenda hilo hata kidogo.

²⁰⁴ Na wakati nilipokuwa nimelala hapo nikiwazia hayo, nikasikia kitu Fulani waziwazi kabisa kama vile unavyoisikia sauti yangu, kama nilivyokuwa nikiwaambia jana usiku, ikasema, “Endelea kukaza mwendo.”

²⁰⁵ Vema, ni—ni...kwanza ni...Linakuja kwa namna fulani, kama tu maono haya hapa: Unalisema, wala hujui ulilisema. Unazungumza, kuongea; hujui unaongea. Ninapoona ono mbele ya mtu, sijui niliyosema. Jinsi tu ninavyojua ni kurudi kwenye kanda hapa na kuyapata. Mnaona? Sijui niliyosema, sababu uko mahali pengine katika sehemu nyingine, labda miaka arobaini, hamsini huko nyuma katika maisha ya mtu fulani, au huko

mbele kabisa katika maisha ya mtu fulani. Unaona? Hujui; hujui kabisa unayasema.

Nami—nami nilisema, “Ninakaza mwendo.”

Kasema, “Endelea kukaza mwendo; endelea kukaza mwendo.” Kasema, “Thawabu kubwa iko mwishoni mwa safari.”

²⁰⁶ Sasa, niliomba ruhusa ya we—wenye viti na kadhalika kusema hivi. Ninaamini lilikuwa ni ono, lakini ikiwa ndivyo, sijawahi kuona kitu kama hicho. Nimeona maono tangu nilipokuwa na umri wa yapata miaka mitatu, labda mdogo kuliko hivyo. Wala sijawahi kuona kitu kama hiki, kamwe sijawa na tukio kama hilo kunitokea. Ninasoma kitabu ambacho mchungaji hapa alinipa, cha mtu mwingine ambaye alikuwa na tukio kama hilo. Nilikisoma, kwa maana ndani yake kilisema Ndugu (Hilo lilikuwa ni lipi? Wigglesworth? Au . . .) Price, Ndugu Price alikuwa na tukio kama hilo; nilitaka kuchukua kitabu chake nione ilikuwa nini. Na—nataka kujua.

²⁰⁷ Sitaki kusema “kuhamishwa,” kwa sababu ingeonekana kama, kama ungesema, ingekuwa ni kujaribu kumwiga Mtakatifu Paulo. Hapana, nataka—nataka kuwa tu vile nilivyo. Mnaona? Ninii tu . . . Siwezi kuwa Mtakatifu Paulo, lakini ninamtumikia Mungu yeye yule aliyemtumikia. Na kwa hivyo . . .

nilisema . . . Iiendelea kusema tu, “Endelea kukaza mwendo.”

Nami ni—ni—nikajibu, nikasema, “Naam, ninakaza mwendo.”

Akasema, “Thawabu kubwa iko kwenye mwisho wa safari.”

Nikasema, “Ninatambua . . .” Nikasema, “Nani . . . Hapana shaka huyo alikuwa ni mke wangu.” Nikasema, “Ulisema nini, mpenzi?”

Nilimtikisa; nikasema, “Meda? Ulisema nini?”

Akasema, “Huh?” Alikuwa amelala.

²⁰⁸ Nami nikasema, “Vema haikuwa ni yeye.” Nikasema, “Labda huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu.” Nikasema, “Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, je, ulikuwa unazungumza na mtumishi Wako? Je, ungetaka nijue nini?”

²⁰⁹ Hakuna kilichozungumza. Nikangoja kidogo. Nikaisikia tena, ikisema . . . Iionekana kana kwamba ningeweza kusikia mtu akiimba ule wimbo, “Bwana, jalia niangalie ng’ambo ya pazia la wakati.” Mliwahi kuusikia? Mnaujua?

Bwana, jalia niangalie ng’ambo ya pazia la
kivuli, cha huzuni na hofu,
Jalia nisikie kengele tamu za bandarini zikilia;
Ingeangaza njia yangu na ingeondoa hofu zote;

Bwana, jalia niangalie ng'ambo ya pazia la wakati.

Ilionekana kana kwamba ningemsikia mtu akiimba huo. Nikawazia, "Nashangaa hiyo ni nini?" Nilikuwa vile vile, kama nilivyo sasa.

Ndipo nikasikia Kitu kikisema, "Endelea kukaza mwendo."

Nikasema, "Nitaendelea kukaza mwendo."

Akasema, "Je, ungependa kuona ng'ambo ya pazia la wakati?"

Nilisema, "Ingenisaidia."

²¹⁰ Na papo hapo, nilihisi kitu fulani kikitokea kwangu. Nami nikawazia, "Kuna nini hapa?" Nikaangalia nyuma, nami niliweza kujiona nimelala kitandani.

²¹¹ Sasa, ikiwa hili—ikiwa hili linakutatiza, Mungu anisamehe kwa kulisimulia. Unaona? Sijawahi kulisimulia hapo kabla, ila kwa kanisa langu, kanisa langu mwenyewe. Basi nikaangalia nyuma, nami natumai kwa neema ya Mungu, kwamba hutanihesabu kuwa mlokole. Mimi—mimi... Ikiwa ndivyo nilivyo, sijui. Si—sitaki kuwa hivyo. Hapana, bwana. Lakini mimi...Mungu Mbinguni anajua kuwa hii ni kweli, ninapoishikilia Biblia yangu juu yake, kama vile tu nilivyowaambia jana usiku juu ya wale kuchakulo. Hili lilitendeka hivi karibuni tu.

Niliangalia nyuma, nami nikajiona mwenyewe, wala sikuwa nikisogea. Basi nikageuka, nikatazama huku; ilionekana kama mahali padogo pakishuka namna *hii*.

²¹² Na mimi—mimi—mimi nasema hii si kama kuomba msamaha, lakini nimekuwa mkali sana kwa wanawake. Nimeitwa mchukia wanawake, bali sivyo nilivyo; si—sivyo nilivyo. Na—nawapenda dada zangu, lakini sipendi kuona wanawake wakifanya vile wanawake wa kisasa wa Marekani walivyo. Nilipokwenda Saint Angelo, yale mapango ya kuzikia huko Rumi, nchini Italia, kulikuwa na ilani hapo juu makaburini iliyosema, "Tafadhali, wanawake wa Marekani, vaeni nguo zenu kabla ya kuingia mahali hapa na kuwaheshimu wafu." Hmm. Ilani kwa wanawake wa Marekani, mbona, ni aibu.

Waliniuliza, "Hivi hamna wanawake wowote waadilifu huko?"

Nikasema, "Loo, hakika tunao. Hao ni ninii tu...Huo ni umati huo mwingine." Mnaona?

Lakini wanawajua tu kama Wamarekani, hivyo ndivyo ilivyokuwa.

²¹³ Na kwa hiyo, hili...si...sitakuwa na wakati katika mkutano huu kuwaambia. Katika mwaka wa 1933...Hili ni taifa la mwanamke. Ni namba kumi na tatu. Linapatikana

katika mlango wa kumi na tatu wa Ufunuo: nyota kumi na tatu, milia kumi na mitatu, kumi na tatu... Kila kitu ni kumi na tatu. Kila kitu ni mwanamke. Halafu kumbukeni, BWANA ASEMA HIVI kutakuwako na mwanamke atakayetawala kabla ya wakati wa mwisho. Ama atakuwa Rais, Makamu wa Rais, ama itakuwa ni Kanisa Katoliki kama mwanamke. Nimemwona: Mwanamke mashuhuri, taifa lilimwinamia. Atatokea mmoja kabla ya wakati wa mwisho. BWANA ASEMA HIVI. Liandikeni mtafute kujua, ninyi vijana. Angalieni kama litatokea. Kama sivyo, mimi ni nabii wa uongo.

²¹⁴ Sasa, kumbukeni tu; huo ndio mwisho. Marekani hili ni taifa la mwanamke. Ni mahali ambapo yeye ni mungu huria, wala mwanamume hamwambii kitu. Yeye ni kimbelembele; anatawala kila kitu, biashara na kila kitu, hata anaingia kanisani jukwaani, mimbarani, na kuiendesha sasa. Kwa hiyo haya—haya basi, unaona, ni... Na hilo si la kimaandiko kabisa kama—kama vile Kaini na Habili... ama Habili angeweza kuwa... kama Kaini. Bila shaka, mambo haya yote, yeye ni mtawala. Na yeye ni—yeye ni mungu mke. Hiyo ni kweli Marekani.

²¹⁵ Sio ninyi, akina dada, lakini sikuzote nilikuwa mkali kidogo kwao namna hiyo. Na labda ni—niliwazia kidogo ni mkali kupita kiasi, labda, wakati mwingine. Lakini ninawezaje? Kama ninyi—kama ninyi ni wa kiroho, mtalishika sasa hivi. Mnaona? Ni wangepi wenu mnaofikiri mnaelewa ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

²¹⁶ Mwangalieni Eliya. Yeye aliita nini? Asingeweza kujizuia. Alimkemea huyo Yezabeli; sivyo? Vipi... Huyu hapa Yohana Mbatizaji anakuja pamoja na roho ile ile yake. Angewezaje kujizuia kulikemea? “Si haki kwako kumchukua mke wa ndugu yako.” Ilimgharimu kichwa chake. Mnaona? Mnaona? Mungu humchukua mtu Wake, bali kamwe si roho Yake. Mnaona? Inaendelea kusonga. Kule kutangulia kwa Kuja kwa Bwana Yesu, kama alivyonena kule chini mtoni katika—katika mwaka wa 1933 wakati nilipokuwa nikibatiza kule, nanyi mnaona kile kilichokipata. Mnaona? Vile tu hasa Yeye alivyosema lingetukia. Kwa hiyo huwezi kulizuia.

²¹⁷ Ndipo nilipoangalia, wakinikimbilia, ilivyokuwa, ilionekana kwangu, kama wasichana milioni moja, yapata umri wa miaka ishirini. Sijawahi kuona wanawake warembo jinsi hiyo maishani mwangu. Macho yao yalionekana kama nyota, meno yao meupe kama lulu, nywele ndefu zikining’inia hadi viunoni mwao, wamevikwa mavazi meupe hata miguuni mwao, nao walikuwa miguu mitupu. Na kila mmoja wao... Sasa, mimi... Samahani sasa, ninyi wanawake. Kila mmoja wao alikuwa akikimbia na kunikumbatia kwa mikono yao, na kupiga makelele, “Ndugu yetu wa thamani.”

218 Sasa angalieni, Mungu anajua, wakati nilipokuwa mvulana, mlisoma hadithi yangu, nilipokuwa na umri wa miaka saba, Malaika wa Bwana alikutana nami kama kimbunga kwenye kile kichaka siku hiyo na kusema, “Kamwe usivute sigara, kunywa pombe, wala kuuchafua mwili wako.” Kamwe sijavuta sigara maishani mwangu, sijakunywa pombe maishani mwangu, nami nina . . . sikujuana na mwanamke yeyote kimwili ila mke wangu. Na kwa hiyo basi, sikuishi maisha machafu nilipokuwa mwenye dhambi. Pia . . . Lakini mimi . . . Tangu nimekuwa Mkristo nimejaribu kuishi maisha mema niwezavyo kuishi, na Mungu anajua hiyo ni kweli.

219 Na—hebu niseme hili: sijali jinsi mwanamume alivyo mtakatifu, maadamu yeye ni mwanadamu, hawezi kukumbatia jinsia nyingine mikononi mwake, mwanamke, pasipo kuwa na hisia ya kibinadamu. Wala sijali; niambie hivyo, nami nitakwambia unasema uongo. Na kama wewe ni mwanamume mwenye damu nyekundu, kama kweli wewe ni mwa—mwanamume, ndivyo ilivyo; huwezi kujiepusha. Wewe ni mwanadamu. Sisemi utafanya jambo lolote baya, sasa; bali hiyo hisia iko mle vivyo hivyo hasa.

220 Lakini katika jambo hili, ilikuwa imetoweka. Mungu asifiwe, ilikuwa imetoweka. Ilikuwa ni kama—sio kama ninavyomchukua dada yangu mwenyewe, Dolores, mikononi mwangu. Haikuwa kama vile mama akimchukua mtoto wake mchanga. Si—sijui. Ilikuwa ni kamilifu.

221 Ndipo nikaangalia, hili hapa kundi la wanaume likaja, ilionekana kama mamilioni yao wakija kutoka upande huu. Nao wote walikuwa wamevaa mavazi meupe na walikuwa na kama, nywele za matimutimu zikining’inia shingoni mwao. Nao walikuwa wakinishika na kupiga mayowe, “Ndugu yetu wa thamani.”

222 Nikasema, “Si—sijui mimi.” Ndipo nikageuka, nikaangalia, nami yule pale nimelala kitandani. Sasa popote kulipo, sio mbali sana kutoka hapa. Kama ni kiwango kingine ama chochote kile, siwezi kusema. Lakini niliangalia nyuma, nami nikajiona nimelala kitandani; nikaangalia hivi, na hawa hapa watu hawa. Na hiyo . . .

223 Kama ningesema “kamilifu,” hilo lisingetosha. Kama ningesema “adhimu”; nisingeweza kupata neno la Kiingereza. Hakukuwako na jana, hakuna kesho, yote ilikuwa ni sasa; hakuna ugonjwa, hakuna huzuni, hakuna dhambi, hakuna uchovu; hawakula wala kunywa; hawakulala, haikuwabidi kulala; bali hata hivyo walikuwa ni watu. Nao wangenikumbatia, ninahisi tu jinsi ninavyoihisi mikono yangu namna *hii*. [Ndugu Branham anapigapiga mikono yake—Mh.]

224 Ndipo nikaona akipenyeza kupitia kwa huo umati, na huyu hapa mke wangu mpendwa mwenyewe anakuja. Alikufa

alipokuwa na miaka ishirini na miwili naye huyu hapa anakuja, mama wa Billy. Naye akaja moja kwa moja... Nikasema, "Ataniita mumewe."

²²⁵ Alikuwa akipitia kwa wanawake, akinipungia mkono namna *hiyo*. Ningeweza kuyaona hayo macho meusi yaking'ara tu. Alikuwa msichana wa Kijerumani. Akakimbia na kunikumbatia. Akasema, "Ndugu yangu mpendwa."

Na kulikuwako na mwanamke mrembo kweli amesimama pale, akanikumbatia tu na kusema, "Ndugu yetu mpendwa."

Halafu Hope, akanikumbatia (Huyo alikuwa mke wangu.) akamkumbatia mwanamke huyu mwingine; akasema, "Si ajabu hii? Yuko pamoja nasi sasa."

Nikasema, "Si—sielewi hili." Nikasema, "Si—si—siwezi kuele- . . ."

²²⁶ Nao watu hawa wakaninyanyua juu, wakaniweka mahali pakubwa mno parefu, wakaniketisha chini. Nao walikuwa wakimsifu Mungu, hakuna mmoja wao anayenibusu, kunikumbatia tu, na kusema, "Ndugu, ndugu yetu wa thamani."

Ndipo nikaangalia, nao watu walikuwa wakija kutoka kila mahali. Nami nikasema, "Ni nini hiki?"

Ndipo ile Sauti sasa, haitoki kwa yeyote, Sauti ile ile iliyonena chumbani ingali ilikuwa pamoja nami, Yeye akasema, "Huu ni upendo mkamilifu."

²²⁷ Nami daima nimefundisha: Ushahidi wa Roho Mtakatifu ni upendo mkamilifu. Mnaona? Ninaamini katika kunena kwa lugha, hakika. "Lakini nijaponena kwa lugha ya wanadamu na Malaika wala sina upendo, si kitu mimi, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao." Kwa hiyo, unaponena kwa lugha na unao upendo pamoja nayo, hiyo itakuonyesha.

²²⁸ Nao upendo ambao tungekuwa nao hapa ungekuwa ni kama kuanza hapa kutoka kwenye kivuli, cha kivuli, cha kivuli kuingia katika kivuli; na kutoka kwenye kivuli kuingia kwenye ukungu, na kwenye unyevu kidogo, hata kwenye kijito, kuingia mtoni, halafu kuingia baharini. Hapo ndipo unapofikia hapo, mkamilifu tu, kila kitu. Usingeweza kufa; usingekuwa na dhambi yoyote. Loo, kamwe sininii . . . Ka—kamwe nisingeweza kuelezea jinsi Mahali hapo palivyokuwa. Mnaona? Pa—pa—palinii tu . . . Palikuwa pakamilifu, zaidi ya kamilifu. Na papo hapo, kulikuwako na . . .

Nikasema, "Si—sielewi haya ni nini."

Ndipo mwanamke mrembo kwelikweli akanikimbilia na kusema, "Loo, ndugu yangu mpendwa," akasema, "Nina furaha sana umewasili."

Kisha akageuka, nami nikamtazama, ndipo nikawazia, “Jamani, jinsi ambavyo kila mtu ni mrembo sana, na mchanga kweli, na ninii sana...” Kisha nikasema, “Ni kitu gani hiki?”

Nayo ile Sauti ikasema, “Hapa ndani chochote kinachofananisha uzee na kila kitu kinarejeshwa katika ukamilifu.”

²²⁹ Mnaona, tunakula chakula mpaka tunafikia umri fulani. Nilipokuwa na miaka kumi na sita, ningekula cha... Hebu sayansi inijibu hili: Ninakula chakula kile kile nilichokula nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, ninakula sasa: maharage, mkate, viazi, nyama. Na kila nilapo, ninayafanya upya maisha yangu. Kila mtu anajua hiyo inafanyiza seli za damu, na hivyo ndivyo tunavyokuja duniani. Na sasa, daktari anayeketi hapa angejua vivyo hivyo. Ndipo nikawa na nguvu zaidi, nikazidi kuwa mkubwa wakati wote. Ndipo nilipofikisha yapata miaka ishirini na miwili, nawe pia, ningali ninakula chakula kile kile, huku nikizeeka zaidi na kudhoofika wakati wote, nikiweka uhai mpya mwilini mwangu.

²³⁰ Nielezeeni, enyi wanasayansi: Kama ninamimina maji ndani ya bilauri kutoka kwenye jagi, na wakati inapofikia nusu, ninaendelea kumimina zaidi nayo yanaendelea kupungua. Kisayansi, niambieni kuhusu hilo. Jambo ni kwamba, ni miadi aliyoifanya Mungu. Unapofikia umri huo, Yeye amekufikisha mahali anapokutaka, kasema, “Karibu mauti; anza.” Ulizeni sayansi endapo huanzi kufa ukiisha kuwa na yapata umri wa miaka ishirini na miwili. Haidhuru unakula vizuri jinsi gani, unakufa, ukiondoka moja kwa moja. Hatimaye... Mauti yanakuandama papo hapo. Lakini unakua hata utakapoufikia umri huo. Kutoka yapata... Uko katika hali yako iliyo bora zaidi kutoka yapata miaka kumi na mitano hadi yapata ishirini na miwili. Hiyo ni kweli.

²³¹ Watu hawa walionekana kuwa kwenye upeo wao kabisa, kwenye ubora wao. Nami, nikiwaangalia kule na jinsi walivyoonekana. Ili kwamba, niliwazia, “Si ajabu hiyo?”

²³² Ndipo nilipomwona msichana wangu mdogo, mwenye umri wa miaka minane, wakati... Mnakumbuka ule usiku, nanyi mmeisoma katika hadithi yangu. Nilipokutana naye, alikuwa ni msichana. Alisema, “Aloo, Baba.”

Nikasema, “Ati Baba? Mbona, wewe ni wa umri wangu. Sielewi hili.”

Akasema, “Baba, duniani, nilikuwa mtoto wako Sharon.”

Nikasema, “Yu wapi mama yako?”

Kasema, “Yuko huko juu nyumbani mwako akikungojea.” Akasema, “Nitangojea hapa kwa ajili ya Billy Paul, ndugu yangu.”

²³³ Ndipo nilipotoka kwenye hilo ono...Hope alikuwa amenikumbatia Kule, ndipo nilipotoka kwenye hilo ono, nikisimama chumbani, alikuwa bado amenikumbatia. Wala sikuwa katika ono lolote, sio kuzimia; nilikuwa nimesimama kama ninavyosimama sasa. Naye alikuwa akinipapasa kwenye bega hili. Mungu ndiye Hakimu wangu.

Nikasema, "Hope, ungali hapa, sivyo?"

Akasema, "Billy, niahidi kwamba hutahangaika kunihusu mimi pamoja na Sharon."

²³⁴ Nilikuwa karibu ku-...Nilikuwa na bastola mkononi mwangu dakika chache hapo kabla. Nilikuwa nimeinyakua kote kote, nikijaribu kujiua. Siku ile ile, nilijaribu kuweka mkono wangu kwenye waya wa volti elfu thelathini na tatu nilipokuwa nikifanya kazi kama fundi umeme, mnaijua hadithi yangu. Basi muda si muda najua, nilikuwa sakafuni, nimeketi pale, nikitoka jasho, bila kujua kilichotukia. Hilo lilimaanisha Mungu akihiifadhi huduma hii kwa ajili yenu ninyi watu; ningaliondoka papo hapo.

Na kwa hiyo, alikuwa amenikumbatia. Nikasema, "Hope, ungali hapa." Ilikuwa giza chumbani.

Akasema, "Utaniahidi?"

Nikasema, "Ninakuahidi, Hope."

Basi alipofanya hivyo, akaniacha; akanipapasa, kwa namna fulani akanikumbatia, kisha akaniacha.

Nikasema, "Ungali hapa, Hope, mahali fulani, sivyo?" Nikapapasa-papasa kote nikimtafuta. Nikawasha taa, nikaenda kwa kila kiti na kushikashika kote.

²³⁵ Nikasema, "Uko wapi, mpenzi? Usiniache; usiniache." Nikazunguka chumbani, nikipapasapapasa namna hiyo nimpate; mvulana tu, nilikuwa nimeoa muda mfupi, naye Billy na Sharon walikuwa wamezaliwa.

²³⁶ Nami nilimwona. Nilipomwona wakati huu, alionekana vile vile. Nami nilikuwa nimeketi pale katika mahali hapa. Ndipo nikasema, "Sielewi haya. Mbona mkaniweka hapa juu?"

Kasema, "Ulikuwa kiongozi. Ulizaliwa kiongozi, kuwaongoza watu."

Nikasema, "Loo, jamani." Nikasema, "Vema..."

Yeye akasema, "Vema, huu ndio ukamilifu." Kasema, "Hii ni kama wale wazee wetu walipokusanyika pamoja na watu wao."

Nikasema, "Je, hii ni...? Mimi—mimi—mimi—mimi... Kwani hii ni baada ya mauti?"

"Naam." Nikageuka na kuangalia nyuma. Mimi yule pale bado nimelala kitandani. Naye akasema, "Hii ni baada ya mauti."

Basi nikasema, “Loo, basi nimekufa. Vema, hii ni ajabu; hii ni nzuri kwangu kuwa hapa. Ninapenda hii.”

Halafu mwanamke huyu, msichana mrembo kwelikweli ambaye ndio kwanza anikumbatie namna *hiyo*. Kisha kasema, “Endelea tu kukaza mwendo.”

Nami nikasema, “Vema, mbona...siwezi kuelewa.” Nikasema, “Je, hawa wote ni Wabranham?” Ilionekana kama mamilioni yao. Nikasema, “Je, hawa wote ni Wabranham?”

Hiyo Sauti ikasema, “Hao ni waongofu wako.”

Nikasema, “Ati waongofu?”

²³⁷ Kasema, “Unamwona mwanamke yule unayemstaajabia?” Kasema, “Alikuwa amepita miaka tisini ulipomwongoza kwa Kristo. Mwangalie sasa. Si ajabu alipiga makelele, ‘Ndugu yangu wa thamani.’”

²³⁸ Nikasema, “Loo, laiti ningalirudi, laiti ningalipata nafasi. Ningewanyakua; ningewavuta; ningewashawishi. Mnaona? Msiache mtu yeyote aukose huu. Huu ni—huu ni ukamilifu.”

²³⁹ Ndipo mara ghafla, nikaangalia. Nilikuwa na maskini mbwa mmoja. Tulikuwa tukiwinda; alinivalisha nguo, akaniweka shuleni, kuwawinda oposamu, kuwawinda kuuni na kadhalika. Ndipo tulipohamia mjini, polisi mmoja akampa sumu.

²⁴⁰ Nilipolipigapiga kaburi lake, wakati nilipomzika kwenye uwanja wetu wa nyuma, nikasema, “Fritz, kukiwepo na mahali...” Nilikuwa mwenye dhambi, yapata umri wa miaka kumi na saba. Nikasema, “Endapo kuna mahali panapoitwa Mbinguni, utakuwa huko.” Baadaye, nikaongoka. Sikuzote niliwazia...

Sasa...Nilimwambia mtu fulani hili, nao wakasema, “Ati mnyama kuwa Mbinguni.”

²⁴¹ Kweli kabisa kuna wanyama Mbinguni. Ninataka kuwauliza jambo fulani. Kutupilia nje ukosoaji huo upesi sana. Niambieni kilichowapata wale farasi na magari walioshuka wakamchukua Eliya kisha wakapanda juu. Yuko wapi yule farasi ambaye Yesu atakuja naye, akimwendesha, huku vazi Lake limelowa Damu, akimwendesha farasi mweupe? Uh-huh? Wako wapi hao mbwa mwitu na mwana-kondoo watakaokula pamoja, na simba atakayekula nyasi kavu kama fahali? Hao watatoka wapi?

²⁴² Ndipo nikaangalia, akishuka kutoka kilimani, naye huyu hapa maskini Fritz anakuja. Aliniangalia na akakaribia na kunilamba mkononi, nikampapasa. Mara naye Prince, farasi wangu, akaja akaweka shingo yake begani mwangu akaanza kulia.

Nikasema, “Ee, Mungu.” Nikaangalia juu.

Ndipo Yeye akasema, “Wote ambao uliwapenda, na wote waliopata kukupenda wamekusanyika hapa.”

Nami nikasema, “Nataka kumwona Yesu. Nataka kumwona Yule ambaye nimempenda na—na nikamtumikia.”

²⁴³ Nao wakasema, “Huwezi kumwona sasa hivi; Yeye yuko juu zaidi ya *hapa*. Lakini siku moja Yeye atarudi, na atakapokuja, Yeye atakuja kwako kwanza. Nawe utahojiwa juu ya Injili ambayo ulihubiri. Na kisha, kama ukipita huo mtihani, basi tutaenda pamoja nawe, turudi, pamoja Naye, turudi duniani na kuishi pamoja milele katika mwili, mwili wa nyama ambapo tutakula na kunywa.”

Nami nikasema, “Unataka kusema, Yeye atanihoji mimi juu ya Neno nililohubiri?”

Kasema, “Naam.” Nayo ile Sauti iliyosema nami ilisema hilo.

Nikasema, “Vema, hivi Mtakatifu Paulo atahojiwa pia?”

Kasema, “Bila shaka, pamoja na kusanyiko lake.”

Nikasema, “Basi kama Mtakatifu Paulo akiupita, nami pia nitaupita.” Nikasema, “Nimehubiri vile tu alivyofanya hasa, sikuondoka hata neno moja.”

Ndipo basi wale mamilioni wakapaza sauti, “Tunajua hivyo, na tunastarehe tukiwa na hakika.”

Basi yapata wakati huo, nikasikia ile Sauti ikisema, “Endelea kukaza mwendo.”

Ndipo nikajisikia nimeteleza. Nikasema, “Sio lazima nirudi, sivyo?”

“Endelea kukaza mwendo.” Nikageuka na kuuangalia mwili wangu; nikauona ukijongea. Nilikuwa nikijirudia; katika dakika moja nilikuwa humo chumbani tena.

²⁴⁴ Enyi marafiki, tangu wakati huo, nimekuwa mtu aliyebadilika. Sijui mtakaloliwazia hili, bali huku mkono wangu ukiwa juu ya Biblia, hiyo ni kweli. Hiyo... Popote pale, sijui kama ilikuwa ni hapa, kama lilikuwa ni ono. Kamwe sijawahi kuwa na moja kama hilo. Basi hebu tuseme ilikuwa ni kuhamishwa kudogo (Sisemi ndivyo ilivyokuwa), tuseme, roho yangu ilitoka, ikaenda kule (sijui ilikuwa ni kitu gani), kama—kama hilo ni tukufu chini ya Mbingu hiyo ya kwanza, Paulo aliona nini alipoenda kwenye Mbingu ya tatu kisha akarudi na kusema, “Jicho halijaona, sikio halijasikia wala halijaingia mioyoni mwa watu, yale Mungu aliyowawekea akiba hao wampendao.”

²⁴⁵ Nimeyakinia zaidi. Nime... Huu ndio uamsho wangu wa pili tangu wakati huo. Nimeyakinia zaidi kufanya kila niwezacho kuwashawishi wanaume na wanawake, naomba mwe na hakika na hili: Endapo upendo wa Mungu hautii nanga moyoni mwako kabisa, kamwe usichukue hisia yoyote wala mhemuko; hakikisha ya kwamba u—unaweza kugeuza shavu hilo jingine, kwamba—

kwamba Mungu...kwamba—kwamba Kristo ni yote kwako. Kamwe usilikose, ndugu yangu.

²⁴⁶ Kumbuka tu. Nitasema hivi, pamoja na imani niliyo nayo katika hilo ono, chochote lilichokuwa, nitasema hilo katika Jina la Bwana: Isipokuwa uwe na upendo huo mkamilifu, kamwe hutakuwa kule, maana hakuna kitu kingaliweza kuwa kule pasipo na huo. Roho yako ingekuwa haifai kule. Isingekuwa; kusingekuwako na njia kwake kuja. Si zaidi ya vile ingekuwa kwa punje ya mhindi kuchipusha ardhini pasipo na chembe ya uhai ndani yake. Haidhuru ingeonekana ya asili jinsi gani, isingeweza kuchipuka.

²⁴⁷ Rafiki yangu, ninyi wazee, ninyi vijana, hamjui ni wakati gani mtakapoondoka. Hatujui hilo. Lakini hebu nikushawishi, kama ndugu Mkristo, kwamba...anayekupenda: Isipokuwa umezaliwa mara ya pili, naye Roho wa Mungu wa upendo aingie ndani ya moyo wako, hakika utapakosa Mahali hapo. Hebu nikuulize: Kama Mungu amenipa...amenipa kibali kati yetu, nanyi mnaniamini, mimi ni mwaminifu. Ilikuwa? Sijui.

²⁴⁸ Ila Mungu Mbinguni, Yule anaye—Yule aliyeko kila mahali na yupo hapa sasa, nitakapouacha ulimwengu huu, Baba wa Mbinguni, naomba nipumzike humo mpaka Yesu atakapokuja. Hiyo ni...hiyo—hiyo ita—hiyo itakuwa ni thawabu ya kutosha kwangu, ikiwa ninaweza tu kupumzika mahali Hapo, mpaka nitakapomwona Yeye akija.

²⁴⁹ Ndipo ikafunuliwa kwangu, “Kama maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo moja inayongoja tayari”; tunayo moja inayongoja. Ndugu, dada, hiyo ni kweli. Sasa, nafikiri ninaye Roho wa Mungu. Kama Roho aliye juu yangu siye, sijui mimi.

²⁵⁰ Angalieni, hebu tuchukue asili yake. Hebu tuchukue ile Nguzo ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli, ile waliyoipiga picha. Hapana shaka wengi wenu mnayo; kama sivyo, ichukueni wakati mkipita. Ambapo ilichunguzwa na Serikali ya Shirikisho, mawakala wa FBI wa Alama ya Kidole na Hati; iko kule ukumbini. Moja inaning’inia katika Ukumbi wa Kidini wa Sanaa huko Washington, DC, kama Kiumbe pekee cha Kimbinguni kilichopata kupigwa picha. Imeonekana jukwaani. Watakatifu wanaijua; wameiangalia. Mamilioni mara mamilioni kote ulimwenguni wameiangalia ikitenda kazi, wakaiona kibinafsi ikitokea jukwaani.

²⁵¹ Mke wangu, yapata miezi sita iliyopita, aliiona kwa mara yake ya kwanza. Alikuwa mtoni siku hiyo wakati ilipotokea huko chini. Wakati makala ilipoenda kote kwenye u—ulimwengu unaozungumza Kiingereza kwenye Associated Press: *Nuru Ya Ajabu Inatokea Juu Ya Mhudumu Wa Kibaptisti Wa Mtaa Wakati Akibatiza*. Nilisimama hapo, ikanena; watu wakaisikia ikiongea na kujibu. Maelfu ya watu wakisisimama pale wakiniangalia

nikibatiza kutoka kwenye uamsho wangu wa kwanza, waongofu mia tano katika Mto Ohio. Ilikuwa gazetini, mikato ya gazeti; tunayo. Ikaingia kwenye Associated Press; Canada inayo; kote nchini. “Nuru ya Ajabu. . .”

²⁵² Sasa, ulimwengu wa kisayansi umeichukua. Sasa, wameipiga picha mara tatu ama mara nne mbalimbali. Ujerumani wameipiga picha. Waliipigia kule chini California sio muda mrefu uliopita. Hao ni watu halisi wakiwa na kamera halisi.

Kamera ya Ujerumani ilisema, “Tunashangaa kama kamera yetu ingeweza kuipiga?”

Nikasema, “Mnakaribishwa kujaribu.”

²⁵³ Ndipo wakati Roho alipokuwa akishuka chini, walimpiga picha akishuka, wakampiga wakati akifanya upambanuzi, kisha wakaipiga picha wakati ikipaa juu tena. Loo, jamani. Maelfu mara maelfu waliusujudia Msalaba huko Ujerumani. Na huko ndiko nitakaporudi mara watakaponinii. . . Ninapoweza kuwa huru kurudi Ujerumani tena, huko Lausanne, Switzerland, ilikuja tena.

²⁵⁴ Sasa, angalieni asili Yake. Kama mzabibu. . . Kama ukininii. . . Kama tawi la kwanza. . . Yesu alisema, “Mimi ndimi Mzabibu; ninyi ni matawi.” Yohana Mtakatifu 15, ninaamini. Hiyo ni kweli? “Mimi ndimi Mzabibu.”

²⁵⁵ Sasa, huo Mzabibu ulizaa tawi gani? Tawi la kwanza lilikuwa ni kanisa la Kipentekoste. Hiyo ni kweli? Basi tawi la pili litakalotokea litakuwa ni kanisa la Kipentekoste. Sasa, hatuoni Upentekoste katika makanisa yote, sivyo? La. Vema, ni kitu gani? Ni mzabibu uliopandikizwa.

²⁵⁶ Unaweza kuchukua mpichi ama unaweza kuchukua ninii, ningesema, m—mchungwa, na kupandikiza karibu namna yoyote ya tunda la aina ya chungwa. Unaweza kupandikiza karibu chochote, mbalungi ama wowote ule, bali umepandikizwa. Lakini kama ule mzabibu asili ukitoa tawi, litaleta tunda la namna ile ile ambayo lile la kwanza lilileta.

²⁵⁷ Sasa, ikiwa Yesu Kristo ndiye Mzabibu, na Maisha Yake. . . Sasa kumbukeni, ninii Yake. . . Mzabibu hauzai tunda; tawi huzaa tunda, bali linatiwa nguvu na huo mzabibu. Hiyo ni kweli? Vema, basi kama Uhai wa Kristo ukiwa ndani yetu, utamleta Roho Wake na matendo Yake. Hiyo ni kweli? Hauna budi kuleta, kwa sababu ni Mzabibu wa Mungu. Sasa. . .

²⁵⁸ Sasa, mwangalie Malaika huyu wa Bwana. Tunajua ya kwamba hiyo ni kweli. Sasa, angalia ana asili ya aina gani. Anazaa tunda lile lile alilozaa wakati alipokuwa hapa duniani. Sasa, amerudi Kanisani, akizaa tunda lile lile, akifanya Kanisa lingine la Kipentekoste, vile vile tu alivyofanya mara ya kwanza. Sasa, Kanisa hilo lilitia muhuri ushuhuda wao kwa damu yao.

Walikuwa ni watu watauwa; walimpenda Mungu; walidumu nalo.

²⁵⁹ Na lolote mfanyalo, lolote mfanyalo, marafiki, hebu niwaulize, kama mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu, hebu niwaambie jambo fulani: Kamwe msipakose Mahali hapo pa ajabu. Msipakose. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu.

²⁶⁰ Ninashangaa sasa hivi, kabla hatujaenda mbele zaidi katika ibada hii: Kunaye mmoja hapa, wawili, dazani, ni wangapi waliopo hapa ambao wangetaka kusema, “Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi sasa hivi, tangu uliposimulia hili, nimekuwa na hofu kidogo ya mauti, na—na—nataka kuwa na hakikisho hilo, nataka kumwinulia Mungu mkono wangu, na kusema, ‘Uniombee’”?

²⁶¹ Mungu akubariki wewe hapa, mwanangu. Mungu akubariki; Mungu akubariki, wewe, wewe. Naam, wote huko nyuma, Mungu awabariki. Mungu awabariki, kote jengoni, rohani; tunaiona mikono yenu imeinuliwa hapo juu. “Nataka kupata amani hiyo ipitayo ufahamu wote.”

²⁶² Ninakesha, nikiomba. Inua mkono wako. Roho Mtakatifu na anene. Kama ukifa usiku wa leo, utaenda ambako kuna mizunguko na, kuomboleza na kusaga meno? Ama unataka kuingia katika raha ile tamu iliyobarikiwa, katika amani? Ninalisema katika Jina la Bwana, pamoja na upako wa Roho Mtakatifu.

²⁶³ Mungu akubariki, kipenzi. Mungu akubariki huko nyuma; Mungu akubariki, dada. Mtu mwingine? Inua mkono wako. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli, Mungu akubariki.

²⁶⁴ Ninaangalia, ninangojea tu kidogo. Kila mtu huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mkiomba. Vema, endeleeni tu. Mungu akubariki; ninauona mkono wako. Ninaangalia kitu fulani. Mungu akubariki; hilo ni sawa. Vema, mtu mwingine? Ninaendelea tu kungojea. Vema.

²⁶⁵ Baba wa Mbinguni, Wewe unaiona mikono yao. Nilikuwa nikiangalia, nikiangalia kitu fulani kikitendwa, Wewe unajua yote kukihusu, Baba. Ninaomba sasa ya kwamba Roho Wako atakuwa juu yao kwa utamu. Jalia wajue ya kwamba hili ambalo nimesema, jalia iwe kwamba wanaweza kusema, “Tangu wakati huu na kuendelea,” mitazamo yao imebadilika; ule ugumu uliokuwa moyoni mwao umeyeyuka na kutoweka; amani tamu na upendano wa Kiungu umechukua mahali pake. Lijalie, Baba.

²⁶⁶ Jalia kila mmoja wao aupokee ubatizo wa upendo wa Mungu moyoni mwao, hata wangeweza kugeuza shavu la pili, waende maili ya pili, kama Yeye alivyofanya, huku akiwa na mate usoni Mwake na miiba kwenye paji Lake, huku mbingu na nchi zikiwa

mikononi Mwake, akaenda kwa unyenyekevu msalabani apate kufa kwa ajili ya watu waliokuwa wakimwua. Mungu, vipi...

²⁶⁷ Utufanye hivyo, Baba. Iondoe mioyo yao ya mawe kutoka kwetu na uweke moyo halisi, mtamu, mwema ndani yetu; weka Roho ndani yetu kama aliyo nayo Yeye. Jalia Roho wa Mungu atulie juu ya kila mmoja wa hawa; kumekuwako na watu thelathini ama arobaini walioinua mkono wao. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawapa Uzima wa Milele. Jalia kamwe wasikuonee aibu; jalia wakujie Wewe kwa utamu.

²⁶⁸ Jalia watambue sasa, ya kwamba Kitu fulani kiliwafanya wainue mikono yao. Ni kitu gani? Roho Mtakatifu. Roho wa Mungu, aliye juu yao sasa, aliwafanya wainue mikono yao kufanya uamuzi.

²⁶⁹ Jalia usiku huu uwe ndio ule usiku utakaoninii... wanaoweza kusema, "Tangu Jumamosi hiyo usiku kule chini katika ukumbi wa shule hiyo, nilikutana na Mungu. Jambo fulani lilinipata; nimebadilika tangu wakati huo."

²⁷⁰ Tujalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako kama kumbukumbu za ujumbe. Nawe ulisema, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, wala hakuna mmoja wao aliyepotea." Ee Bwana, uliwaambia utawapa Uzima wa Milele na kuwafufua katika siku ya mwisho, ule Uzima wa Milele, ule upendo, ambao ungewaleta katika uwepo wa Mahali hapa pakuu ambapo nilikuwa na majaliwa ya kupaona majuma machache yaliyopita.

²⁷¹ Baba, siwezi kusema ilikuwa ni kitu gani. Sijui mimi. Unaujua moyo wangu, bali mimi ni mwaminifu tu katika yale nisemayo, Wewe unanishuhudia, Baba. Nami nitaninii... Ni mahali pazuri sana. Mungu, siku zangu zitakapomalizika, ningetaka kumwona mtoto Joseph akiwa ni mtu ambaye ningeweza kuiweka Biblia hii mkononi mwake. Kwa sababu ile siku ya kuwekwa wakfu kwake, Wewe ulinena, ukasema, "Joseph, wewe ni nabii." Ninaomba, Mungu, ya kwamba utajalia sehemu maradufu ya Roho juu ya mvulana wangu. Kama utanijalia tu kuishi na kukuletea watu mpaka nitakapokuwa mzee, halafu niweke Biblia hii mikononi mwa mwanangu, Joseph, na kumwambia aendelee na Injili ile ile, yangekuwa ni maisha makamilifu, Baba.

²⁷² Hata hivyo utakapokuwa tayari kwa ajili yangu, amina. Ni raha ya kupendeza jinsi gani; na—natamani kupaona mahali hapo tena. Bwana Yesu, jalia kila mtu aliye hapa usiku wa leo, kila mtu ambaye ameusikia huu ujumbe usiku wa leo, jalia kusiwe na mmoja wao atakayepotea. Lakini jalia kila mmoja, niwaone kule.

²⁷³ Halafu, tutakapokimbia na kukumbatiana kwa mikono, wakati hakuna tofauti, basi, kati ya mwanamume na mwanamke, hakuna tofauti; u—u—ule mchirizi wa dhambi umeondolewa. Sisi kweli, wakati huo, ni ndugu na dada,

ambapo tunaweza kuishi, dhambi haiwezi kuingia tena, hakuna mawazo mabaya, hakuna chochote kinachoweza kuja mahali pa namna hiyo. Hakuwezi kuwa na unajisi. Sote tutakuwa mmoja katika Kristo.

²⁷⁴ Jalia tuonekane kule, Bwana. Jalia hawa wanawake na wanaume wazee watambue ya kwamba nimewaambia ukweli. Ni—ni—ni kweli. Jalia vijana hawa wadogo wayanyoshe maisha yao, wanaosimama kwenye njia panda usiku wa leo, jalia wachague njia inayofaa hata kusiwe na huzuni kwenye siku ya kuondoka. Tujalie, Baba. Ninawakabidhi mikononi Mwako sasa, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

²⁷⁵ Mnajisikia vizuri sana? Mnaamini ya kwamba Roho wa Mungu aliwafanya mwinue mkono wenu? Hebu tuone. Mnaamini hivyo? Mnaamini linatoka kwa Mungu? Niliwaambia kutoka moyoni mwangu.

Nilipozungumza na rabi mmoja hapa si muda mrefu uliopita, alisema, “Bw. Branham, ninyi mnamwita Mwana wa Mungu,” kasema, “na iwe mbali na Mungu kuwa na mwana.”

Nikasema, “Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu.”

Kasema, “Ati Mungu kuwa na mwana? Yeye hakuwa Yesu wala Kristo.” Kasema, “Yeye angeweza kuwa Yesu, bali hakuwa ni Kristo.” Hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Nikasema, “Bwana, ungewaamini manabii?”

Yeye akasema, “Naam, hakika naamini manabii.” Yeye alikuwa rabi, rabi wa Kiyahudi, Benton Harbor, Michigan.

²⁷⁶ Nikasema... John Rhyn alikuwa ameponywa, kipofu kwa muda wa miaka ishirini, ameketi mtaani. Akasema, “Nilimpa John sadaka nyingi.” Akasema, “Ni—ni nguvu gani, ni kwa mamlaka gani ulimfungua macho?”

Nikasema, “Kamwe sikumfungua macho. Yeye alipata kuona kwa imani katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.”

Akasema, “Mwana yupi wa Mungu? Mungu angewezaje kuwa na mwana?”

Nami nikasema, “Yeye alikuwa na Mwana.” Nikasema, “Je, unaamini Isaya 9:6?”

Kasema, “Hakika.”

Nikasema, “Nabii huyo alikuwa akinena juu ya nani? Masihi?”

Kasema, “Naam.”

Nikasema, “Masihi atakuwa na uhusiano ga—gani na Mungu?”

Akasema, “Yeye alikuwa ni Mungu. Atakuwa ni Mungu.”

²⁷⁷ Nikasema, “Vivyo hivyo na Yesu. Yeye alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili na—na akakaa miongoni mwetu. Mungu

alijidhihirisha Mwenyewe katika mwili. Yeye—Yeye alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili; Roho wa Mungu aliishi ndani Yake katika utimilifu. Sisi tunaye kwa kipimo.”

²⁷⁸ Nasi tunayaangalia Maisha Yake. Sasa, Roho wa Mungu yuko ndani yetu, lakini jambo ni kwamba: kamwe hatuwezi kufungua mifereji hiyo iliyofungamana kumruhusu Roho amiminike ndani. Sasa, Roho wa Mungu, kama angalikuwa kanisani usiku wa leo, angemshuhudia Roho wa Mungu. Hiyo ni kweli?

Kuna kadi zozote za maombi mkutanoni? (Je, alisambaza kadi za maombi? Hapana?) Kuna kadi za maombi? Hapana, hakuna kadi za maombi.

²⁷⁹ Lakini kunaye Mungu: Jina Lake ni Yesu Kristo. Yeye ni Mwana wa Mungu. Ninaamini ninao upako Wake. Ujumbe ambao nimewahubiri, endapo ni wa Mungu, hebu Mungu alithibitishe Neno Lake Mwenyewe. Sikukusudia kufanya hivi, bali ni—ninahisi dharura ya hili kabla sijasema jambo lingine.

Ni wagonjwa wangapi waliopo hapa ndani? Inua mkono wako, kwamba wewe ni mgonjwa na unamhitaji Mungu, inua mkono wako. Inua tu mkono wako, useme, “Ninaamini.”

²⁸⁰ Unaamini? Kama Mungu atakuja hapa na kufanya kazi zile zile alizofanya... Ni wangapi wanaamini ya kwamba Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu sasa hivi? Kitabu cha Waebrania, hiyo ni kweli, ndugu? Hiyo ni kweli? Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Ni wangapi wanajua hiyo ni Biblia? Yeye yuko hivyo lini? Sasa hivi; vema, kama ndivyo alivyo, Biblia ilisema, Waebrania 13:8, “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Hiyo ni kweli? Vema. Ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, basi yeye yule jana, leo, na hata milele, kama ukimgusa, Yeye angetendaje leo hii? Ikiwa Yeye ni yule yule, angetenda vile vile. Hiyo ni kweli?

²⁸¹ Basi mwanamke wakati mmoja, alijipenyeza kupitia kwenye umati na kuligusa vazi Lake, na kujisikia mwenyewe ya kwamba alikuwa ameponywa, ndipo akatoka, akaketi kwenye umati.

Watu wengi walikuwa wakimgusa, wakisema, “Loo, aloo Rabi. Tuna furaha kuwa na Wewe hapa,” na kadhalika. Ndipo basi mwanamke huyu...

²⁸² Yesu alisema, “Ni nani aliyenigusa?” Petro akamkemea, bali Yeye akasema, “Naona kuwa nguvu, uweza, umenitoka.” Akaangalia pande zote kwenye kusanyiko mpaka akampata maskini mwanamke huyo, akamwambia alikuwa anatokwa na damu nayo imani yake ilikuwa imemwoko. Hiyo ni kweli?

²⁸³ Vema sasa, endapo Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, hivi Yeye hatafanya jambo lile lile usiku wa leo kama akiguswa? Sasa, Yeye angefanyaje jambo hilo? Yeye ni Mzabibu sasa; sisi ni matawi. Hiyo ni kweli? Vema, basi, Yeye angetenda kupitia kwa tawi.

Endapo ni tawi zuri kutoka kwa Mzabibu, lingetenda kazi vile vile kama Uhai uliokuwamo ndani ya Mzabibu. Hiyo ni kweli? Sasa, ninyi ombeni; aminini.

²⁸⁴ Ninaomba; ninaamini. Na juu ya msimamo ambao nimechukua kwa ajili ya Mungu kote duniani; na huduma hii ya upambanuzi sasa inaondoka, nami ninaingia katika huduma kubwa zaidi ya kunena Neno. Nanyi mnaona yale Mungu amefanya? Yeye ameliweka moja kwa moja mikononi mwa watu tena. Acha waje na mtazamo mzuri na mwone litakalotukia, bali inawabidi wao kuwa na mtazamo wa kweli. Mnaona, mnaona? Mnaona, hakuna mtu anayeweza kuponya; Yeye ndiye Mponyaji. Bali siwezi kulisema mpaka Yeye aseme nami, mnaona? Lakini unaweza kunena sasa pamoja na imani yako na kupata uponyaji wako kama utaamini.

Wewe ninii tu, wewe anza kuomba moyoni mwako, “Bwana, jalia aseme na mimi.” Uone litakalotukia.

²⁸⁵ Na kama atalifanya, ninataka kila mmoja uliyeinua mkono wako, aje hapa na kusimama kuyazunguka madhabahu na tufanye amani yetu sawa na Mungu. Wewe omba, kuwa na imani.

²⁸⁶ Sasa, Baba wa Mbinguni, baada ya kuhubiri namna hiyo, hii ni . . . badiliko kwelikweli. Naomba, Baba, ya kwamba Wewe utanipa nguvu kujistarehesha mwenyewe na kuwastarehesha watu huko nje, hata sisi, pamoja, tuweze kumruhusu Roho Wako atende kazi kupitia kwetu. Ingetufaa kiasi gani kama ulitenda kazi kupitia kwangu, wala sio kupitia kwao? Kusingekuwako na jibu. Ulikuwa kwenye mji Wako Mwenyewe, ambamo ulilelewa, nao walichukizwa Nawe. Nawe ukasema, “Miujiza mingi usingeweza kufanya,” kwa sababu ya kutokuamini kwao. Wewe ni yeye yule usiku wa leo, kwa kuwa Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Jalia kutokuamini kwote kuondolewe. Jalia wao. . . Kama kutokuamini kukinigusa na kusema, “Haitafanya kazi usiku wa leo,” ninakukataa. Yeye aliniahidi, nami ninamwamini. Sasa, jalia kutokuamini kuondoke kwenye jengo hili, na jalia Kristo ajithibitishe Mwenyewe kuwa hai kama vile alivyosema angefanya.

²⁸⁷ Ndipo, Baba, kama mwisho ukija ifikapo asubuhi, basi, Bwana, wataondoka bila udhuru. Kwamba watu hawa, walioinua mikono yao, na wanakutaka Wewe, waweze kujua kwamba ni Roho wa kweli wa Mungu anayesema nao humu jengoni usiku wa leo, tunavikabidhi vitu hivi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁸⁸ Sasa, nachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo, ama, mamlaka ya Roho Mtakatifu. Sasa, ninyi ombeni.

²⁸⁹ Kuna mama anayeketi papa hapa nyuma, wa pili ndani, papa hapa, ana tatizo la figo, anaombea uponyaji wake. Unataka kuponywa, mama? Unaamini ya kwamba Mungu atakupaa

afya? Unaukubali? Vema, inua mkono wako basi. Nenda zako nyumbani upate afya.

Mwulize huyo mwanamke kama hakuwa akiombea ugonjwa wake wa figo. Hiyo ni kweli.

Hiyo ni kweli, mama? Hiyo ni kweli, inua mkono wako, watu wapate kuona.

Sasa, hana kadi ya maombi. Simjui huyo mwanamke; sijawahi kumwona maishani mwangu.

Hiyo ni kweli, mama? Ikiwa hatufahamiani mmoja kwa mwingine, pungu mkono wako.

Sasa, una imani ya kuamini.

²⁹⁰ Hiyo inamfanya Yeye yule yule? Huyo mwanamke alifanya nini? Alimgusa Kuhani Mkuu; huyo Kuhani Mkuu akanena kupitia kwangu na kuonyesha ono, vile hasa Yeye alivyosema angefanya.

²⁹¹ Yesu alisema, “Sitendi neno, ninii tu. . .” Yohana Mtakatifu 5:19. “Amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe; ila lile amwonalo Baba akilifanya, ndilo atendalo Mwana vile vile.” Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua hiyo ni Maandiko? Yohana Mtakatifu 5:19. Ombeni, ombeni tu; ombeni kwa unyenyekevu.

²⁹² Hapa, nimemwona mwanamke mkongwe ameketi papa hapa nyuma, papa hapa sambamba na kidole changu. Hivi hamwioni ile Nuru inayoning’inia juu ya huyo mwanamke papa hapa? Angalieni pale; geuza tu kichwa chako uangalie papa hapa. Huyo mwanamke aliinua kichwa chake. Kidogo ni mzee; ana nywele zenye mvi. Ana tatizo la jicho lake. Amekuwa na mto- . . . ana mtoto wa jicho jichoni mwake, nao watajaribu kumwondoa. Naye amekuwa na upasuaji wa mtoto wa jicho hapo awali. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

²⁹³ Sasa, mama, hiyo ni kweli, sivyo? Ikiwa hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Ikiwa hatufahamiani, pungu mkono wako. Haya basi. Sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, kuwa na imani; mwamini tu Mungu.

²⁹⁴ Sasa, yeye aligusa nini? Alimgusa Kuhani Mkuu. Kama utaamini, mambo yote yanawezekana. Kama unaweza kuamini; mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio. Ninaangalia; endeeleni tu kuomba popote mlipo, roshani ama popote mlipo, haijalishi. Endeeleni kuomba. Semeni tu, “Bwana, nikumbuke. Mimi ni mgonjwa.”

Sasa, usijaribu kujitia wasiwasi. Sema tu, “Bwana, ninaamini mtu huyu anasema kweli. Ninaamini.”

²⁹⁵ Sasa unaona, yule Malaika aliniambia nini? “Kama unaweza kuwafanya watu wakuamini. . .” Sio kuniamini mimi kama mtu, aminini Ujumbe ninaowaambia. “. . . kukuamini wewe, na uwe

mwaminifu unapoomba, hakuna chochote kitakachosimama mbele ya maombi yako.” Hivyo ndivyo huyo Mtu alivyoniambia.

²⁹⁶ Ninamwona mwanamke akilia, akipangusa machozi kutoka machoni mwake. Kama ataniamini mimi kama nabii wa Mungu, ameketi papa hapa mbele yangu, Mungu atamponya. Sikujui, kamwe sijawahi kukuona. Lakini wewe hutoki hapa; unatoka Grants Pass. Kama utaamini kwa moyo wako wote, utaponywa.

Mungu, ataukosa; usiache aukose, Bwana.

Bibi Kruger? Ninakupa changamoto kumwamini Yeye. Kuwa na imani.

²⁹⁷ Simjui mwanamke huyo; sijawahi kumwona maishani mwangu, Mungu anajua hilo. Hakuna njia ulimwenguni kwangu kumjua. Yeye ni mwanamke tu anayeketi pale.

²⁹⁸ Kama hatufahamiani, mama, inua mkono wako. Vema. Um-hum. Vema, chochote alichokwambia, hiyo ni kweli? Punga mkono wako huku na huko namna hii. Vema. Unaamini?

²⁹⁹ Ninamwona mwanamke ameketi nyuma kabisa hapa. Amevaa nguo yenye madoa meupe. Ana kivimbe upande wake wa kushoto. Kuwa na imani; usitie shaka. Usiukose. Mungu. . . Bibi Griffith, mwamini Mungu. Amini kwa moyo wako wote naye Mwenyezi Mungu atakuponya na kukupa afya.

Sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Unafikiria nini juu yake?

Unaamini Mungu anaweza kuponya, dada? Hakika Yeye huponya. Unaamini huo utaondoka, ninii yako...? Vema, anaweza kupata ulichoomba. Um-hum.

³⁰⁰ Sasa, unamwamini Yeye? Basi Roho ambaye alinipeleka kule ni Roho yeye yule anayegeukia hapa, ambaye ulimwengu wa kisayansi wanaye, mara ya kwanza Kiumbe cha Kimbinguni kilipopata kupigwa picha. Ni Nguzo kubwa ya Moto kama ile iliyowaongoza wana wa Israeli, Hii hapa ikitutia mafuta usiku wa leo, ikifanya kazi zile zile ilizofanya wakati Yesu Kriso alipokuwa duniani.

³⁰¹ “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena,” alisema Yesu, “lakini ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi, ‘Mimi’ ni kiwakilishi nafsi, Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

³⁰² Enyi watu (Ee, Mungu!), hivi hamwezi kutambua? Usimtilie maanani maskini mtu huyu mdogo mwenye upara, mabega yaliyoinama, anayesimama hapa akijaribu kuwaambia mambo haya. Msiniangalie mimi, mtu asiye na elimu, mshamba; usiangalie hilo. Angalieni asili ya Roho anayetenda kazi kupitia hapa. Mwaminini Bwana Yesu! Si mimi; sikujui, sijui lolote kukuhusu. Ni Yeye, Kristo akilitimiza Neno Lake kwa yale Yeye aliyosema angefanya.

³⁰³ Kumbukeni, mwisho unakaribia. Tafuteni kimbilio wakati mkiweza, wakati milango ya rehema imefunguliwa kwa ajili ya Mataifa. Tafuteni kimbilio; hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

³⁰⁴ Ninamwalika kila mmoja wenu asiye na imani ile ambayo ingekupeleka kule, aje hapa, asimame karibu na madhabahu haya. Kila mwenye dhambi hapa ndani, kila aliyerudi nyuma, ninataka uje na kusimama hapa karibu na madhabahu. Ikiwa Roho wa Mungu yuko hapa ambaye anakujua, hakika Yeye angejua la kufanya.

³⁰⁵ Mungu akubariki, bwana. Simama uje hapa; angalia jinsi ulivyo mwaminifu. Ungeweza kutembea kutoka huko nyuma kuja hapa, kama ingemaanisha tofauti kati ya kwenda Mbinguni ama kuupoteza wokovu wako?

Unasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa. Nimezaliwa mara ya pili."

Hivi una ule upendo, una uhakika? Usibahatishe juu ya huo. Hebu tuimbe sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza (Mungu akubariki,
ndugu yangu.)
Na kununua wokovu wangu
Kule Kalvari.

Hebu kila mwenye dhambi aje sasa. Utasimama hapa? Haijalishi ushirika wako wa kanisa, kanuni yako ya imani, rangi yako, yeyote uliye.

³⁰⁶ Mungu akubariki, jamaa mdogo. Bwana na akufanye mhubiri. Vema, njoo. Utakuja sasa, hata kabla hatujaimba huo wimbo? Wewe uliyeinua mkono wako, unataka kupata amani hiyo, njoo; amani ipitayo ufahamu wote. Hivi hutakuja?

Nampenda,
Naam, inahitaji upendo Wake kukupeleka kule.
Na . . .
Simameni juu sasa na mshuke hapa chini, sivyo?
Kwani . . .
Na . . .

Si mje? Kulikuwako na yapata mikono thelathini iliyoinuliwa.

. . . Wokovu
Mtini Kalvari.

Sasa, hebu kidogo. Mungu awabariki ninyi mnaosimama hapa, ninyi wanaume watatu. Nilidhani wanawake waliongoza njia.

³⁰⁷ Sikilizeni! Hapa ni kwa kanisa! Hapa ni katika Jina la Bwana! Ninatabiri! Hiyo ndiyo sababu hatuwezi kuwa na

uamsho; hiyo ndiyo sababu Roho wa Mungu hawezi kutenda kazi katika kusanyiko; hiyo ndiyo sababu huduma yangu ina- . . . ninii, inavyoonekana, haipendwi sana na watu: Roho Mtakatifu anakuja na kuthibitisha kila kitu alichosema Yeye angefanya, nao watu watainua mikono yao na watabaki vitini mwao. Huo si uaminifu.

³⁰⁸ Basi mnawezaje kutarajia kuwa na ibada ya uponyaji? Mnawezaje kulitarajia kanisa kufikia ukamilifu wake, wakati watu thelathini watainua mikono yao na watatu watakuja?

Lisikieni! Hiyo ni katika Jina la Bwana: Marekani imeiona siku yake; haitainuka tena. Inaporomoka. Ninanena katika Jina la Bwana.

Na . . . (Ubarikiwe . . . ? . . .) 

60-0716 Tangu Wakati Huo
Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Klamath Union
Klamath Falls, Oregon Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org